BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA WA MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A (GATCE) 2019

## 621 KISWAHILI

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A MEI

# (GATCE) 2019

## 621 KISWAHILI

*Kimechapwa na:*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P 2624, Dar es Salaam,
Tanzania.

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2019**

Haki zote zimehifadhiwa.

# YALIYOMO

DIBAJI V

1.0 UTANGULIZI ........................................................................... 1

2.0 TATHMINI YA KILA SWALI ................................................................ 2

2.1 SEHEMU A: Maswali ya Majibu Mafupi (Taaluma na Ufundishaji)............ 2

2.1.1 Swali la 1: Maandalizi ya Kufundishia Somo la Kiswahili.................2

2.1.2 Swali la 2: Sarufi ..........................................................................4

2.1.3 Swali la 3: Uchambuzi wa Vifaa vya Mtaala wa Kiswahili ................7

2.1.4 Swali la 4: Fasihi Simulizi...............................................................10

2.1.5 Swali la 5: Zana za Kufundishia na Kujifunzia .................................13

2.1.6 Swali la 6: Utungaji .......................................................................15

2.1.7 Swali la 7: Maandalizi ya Kufundishia Somo la Kiswahili................17

2.1.8 Swali la 8:Utungaji ........................................................................20

2.1.9 Swali la 9: Maandalizi ya Ufundishaji ..............................................23

2.1.10 Swali la 10: Stadi za Lugha ...........................................................25

2.2 SEHEMU B: Maswali ya Insha (Taaluma) ............................................... **28**

2.2.1 Swali la 11: Fasihi Simulizi...............................................................28

2.2.2 Swali la 12: Utungaji .......................................................................33

2.2.3 Swali la 13: Sarufi ..........................................................................38

2.3 SEHEMU C: Maswali ya Insha (Ufundishaji) ............................................ **42**

2.3.1 Swali la 14: Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili .. ...........................................................................................43

2.3.2 Swali la 15: Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili .. ...........................................................................................47

2.3.3 Swali la 16: Zana za Kufundishia na Kujifunzia ...............................51

3.0 UCHAMBUZI WA KUFAULU KWA WATAHINIWA KWA MADA..... **55**

4.0 HITIMISHO ................................................................................ **56**

5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO.......................................................... **57**

KIAMBATISHO A............................................................................58

KIAMBATISHO B ............................................................................ **59**

# DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania lina furaha kuupatia umma kitabu hiki kama taarifa ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani wa kuhitimu Ualimu Daraja la A kwa somo la Kiswahili 2019.

Kitabu hiki kinaonesha mafanikio ya mfumo wa elimu kwa ujumla hasa katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Kimsingi, uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani huu ni udhibitisho dhahiri wa namna mfumo wa elimu ulivyofanikiwa au ulivyoshindwa kuwapa watahiniwa maarifa walipokuwa katika mafunzo ya Ualimu Daraja la A.

Taarifa hii inaweka bayana sababu za watahiniwa kupata alama za juu, wastani au alama hafifu. Vilevile, taarifa hii inaonesha baadhi ya sababu zilizowafanya watahiniwa wengi kufanya vizuri kama vile kuelewa matakwa ya swali, kuwa na maarifa na ujuzi katika kujieleza kwa ufasaha pamoja na uelewa wa juu katika mada mbalimbali zilizotahiniwa. Aidha, sababu za baadhi ya watahiniwa kupata alama hafifu zimefafanuliwa pia. Miongoni mwa sababu hizo ni kushindwa kuelewa matakwa ya swali, uelewa mdogo wa watahiniwa katika mada zilizotahiniwa na uwezo mdogo wa watahiniwa katika kujieleza kwa ufasaha.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatarajia kuwa, taarifa hii itakuwa nyenzo muhimu kwa viongozi wa elimu, wakufunzi na walimu tarajali katika kupata mbinu sahihi za kuboresha viwango vya kufaulu vya watahiniwa katika mitihani ijayo.

Mwisho, Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kuwashukuru Maafisa Mitihani, wakufunzi wa somo na wengine wote waliohusika kutayarisha taarifa hii. Aidha, shukurani za pekee ziwaendee wafanyakazi wa kurugenzi ya Utafiti na Tathmini pamoja na kurugenzi ya huduma za kompyuta kwa kushiriki katika uchakataji wa data zilizotumika katika taarifa hii.



Dkt. Charles Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inachambua kufaulu kwa watahiniwa katika mtihani wa Ualimu Daraja la A kwa somo la Kiswahili uliofanyika Mei, 2019 kwa kila swali. Mtihani huu ulikuwa na jumla ya maswali kumi na sita (16) yaliyogawanyika katika sehemu **A**, **B** na **C** kwa kuzingatia mada za *Taaluma* na *Ufundishaji*. Sehemu A ilikuwa na maswali kumi (10) ya majibu mafupi. Maswali hayo yalitungwa kutoka katika mada za muhtasari wa *Taaluma* na *Ufundishaji*. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote. Kila swali lilikuwa na alama nne (4), hivyo, kufanya sehemu hii kuwa na jumla ya alama arobaini (40). Sehemu B ilikuwa na maswali matatu (3) ya insha ambayo yalihusu mada za *Taaluma*. Kila swali lilikuwa na alama kumi na tano (15) ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali mawili (2) na kufanya sehemu hii kuwa na jumla ya alama thelathini (30). Aidha, sehemu C ilikuwa na jumla ya maswali matatu (3) ya insha. Maswali hayo yalihusu mada za *Ufundishaji*. Kila swali lilikuwa na alama kumi na tano (15) na mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali mawili (2). Hivyo, sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama thelathini (30). Kwa ujumla, mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali kumi na manne (14) kati ya maswali kumi na sita (16).

Hata hivyo, mtihani huu ulikuwa na viwango vitatu vya kufaulu ambavyo ni kiwango kizuri kilichoanzia alama 70 hadi 100, kiwango cha wastani kilichoanzia alama 40 hadi 69 na kiwango hafifu ambacho kilianzia alama 0 hadi 39. Aidha, chati za viwango vya kufaulu zimeambatanishwa ili kufafanua kiwango cha kufaulu cha watahiniwa. Rangi ya kijani inawakilisha kiwango kizuri cha kufaulu, rangi ya njano wastani na rangi nyekundu ni kiwango hafifu cha kufaulu.

Jumla ya watahiniwa 4,407 walisajiliwa kufanya mtihani wa 621 Kiswahili kwa mwaka 2019. Kati yao, watahiniwa 4,371 sawa na asilimia 99.1 walifanya mtihani huu. Aidha, watahiniwa 36 sawa na asilimia 0.9 hawakufanya. Kiwango cha jumla cha kufaulu cha watahiniwa katika somo hili ni kizuri kwa sababu asilimia 99.98 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walifaulu kwa daraja A hadi D.

## 2.0 TATHMINI YA KILA SWALI


### 2.1 SEHEMU A: Maswali ya Majibu mafupi (Taaluma na Ufundishaji)

Sehemu hii ilikuwa na maswali kumi (10) yaliyohitaji majibu mafupi ambayo yalitungwa kutoka katika mada za *Taaluma* na *Ufundishaji*. Mtahiniwa alipaswa kujibu maswali yote. Kila swali lilikuwa na uzito wa alama nne (4) hivyo, kufanya sehemu hii kuwa na jumla ya alama arobaini (40). Aidha, kufaulu kwa watahiniwa kumegawanyika katika makundi matatu ambapo, mtahiniwa alipata kiwango hafifu cha kufaulu endapo alipata alama 0 hadi 1.5, 2 hadi 2.5 wastani na 3 hadi 4 kizuri.

#### 2.1.1 Swali la 1: Maandalizi ya Kufundishia Somo la Kiswahili


Swali hili lilitungwa kutoka katika mada ya *Maandalizi ya Kufundishia Somo la Kiswahili* ambapo lilipima maarifa ya mtahiniwa juu ya Kuandaa Azimio la Kazi. Aidha, mtahiniwa alitakiwa kuainisha mambo manne atakayozingatia mwalimu katika upangaji wa mada za Muhtasari katika Azimio la Kazi.

Swali lilijibiwa na asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani na lilikuwa ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vibaya kwani ni asilimia 25.1 pekee ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani na zaidi. Chati Na. 1 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa katika asilimia.




**Chati Na. 1:** *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Watahiniwa 3,275 sawa na asilimia 74.9 waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 1.5. Baadhi yao walishindwa kuelewa matakwa ya swali kwani walitoa hoja ambazo ni tofauti na hoja zilizotarajiwa na kupata alama 0. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliainisha vifaa muhimu vinavyotumika kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji shuleni ambavyo ni *kalenda ya shule, kalenda ya mwaka, muhtasri wa somo na kitabu cha kiada* badala ya mambo manne atakayozingatia mwalimu katika upangaji wa mada za Muhtasari katika Azimio la Kazi ambayo ni: *kuanza na mada rahisi kwenda ngumu, kuzingatia uhusiano uliopo baina ya mada moja na nyingine, uelewa wa walengwa kuhusu mada husika, mazingira ya shule na haja na matakwa ya wanafunzi*. Vile vile, watahiniwa wengine waliainisha mambo mengine ambayo ni kinyume kabisa na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama *kuzingatia idadi ya vipindi, likizo katika muhula, kuanza mada yenye kushikika kisha mada yenye kufikirika pia kuanza na mada halisi kwenda mada isiyo halisi.* Aidha, watahiniwa wengine waliainisha jambo moja kwa usahihi badala ya mambo manne atakayozingatia mwalimu katika upangaji wa mada za Muhtasari na hivyo kupata alama za chini. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika kuwa *hutegemea na matakwa ya wanafunzi, umbali wa shule, jamii inayozunguka na maswala muhimu ya kielimu* na kupata alama 1. Hii inadhihirisha kuwa, mtahiniwa huyo hakuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Maandalizi ya Kufundishia Somo la Kiswahili*. Kielelezo Na. 1.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kinyume na matakwa ya swali.


1. Mambo atakayozingatia mwalimu katika upangaji wa mada za muhutasari katika Azimio la kazi ni


(i) Kalenda ya shule
(ii) Kalenda ya mwaka
(iii) Muhtasari wa somo
(iv) Kitabu cha kiada.

**Kielelezo Na. 1.1:** Majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 1.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali kwa usahihi kwa sababu aliainisha vifaa muhimu vinavyotumika kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji badala ya mambo manne atakayozingatia mwalimu katika upangaji wa mada za muhtasari katika azimio la kazi.

Vilevile, asilimia 20.5 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 2 hadi 2.5 kutokana na kuandika majibu yasiyojitosheleza vizuri. Baadhi ya watahiniwa katika kundi hili waliainisha hoja 2 badala ya 4 kama swali lilivyotaka na wengine waliainisha hoja 2 sahihi na zingine hazikuwa sahihi hivyo, kupata alama za wastani.

Aidha, asilimia 4.6 ya watahiniwa walipata alama za juu kuanzia 3 hadi 4. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Maandalizi ya Kufundishia Somo la Kiswahili* na walielewa vyema matakwa ya swali. Waliweza kuainisha mambo matatu hadi manne atakayozingatia mwalimu katika upangaji wa mada za Muhtasari katika Azimio la Kazi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alianisha mambo hayo kuwa ni: *kuanza na mada rahisi kwenda ngumu, kuzingatia uhusiano uliopo baina ya mada moja na nyingine, uelewa wa walengwa kuhusu mada husika* na *mazingira.* Kielelezo Na.1.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali vizuri.


1 (i) Kuzingatia kuanza na Mada rahisi kwenda ngumu.
(ii) Kuzingatia Uhusiano Uliopo baina ya Mada moja na nyingine.
(iii) Uelewa wa Walengwa kuhusu Mada husika.
(iv) Mazingira.

**Kielelezo Na. 1.2:** Majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi.


Kielelezo Na. 1.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuainisha mambo manne ya kuzingatia katika upangaji wa mada za muhtasari katika azimio la kazi kutokana na kuelewa matakwa ya swali.

### 2.1.2 Swali la 2: Sarufi

Swali hili lilihusu mada ya *Sarufi* ambapo lililenga kupima uelewa wa mtahiniwa juu ya aina mbalimbali za maneno. Swali lilikuwa na vipengele viwili ambapo mtahiniwa alitakiwa kutumia mifano miwili kwa kila moja, kueleza maana ya aina za maneno alizopewa ambazo ni: (a) Vivumishi na (b) Viwakilishi.

Swali lilijibiwa na asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani na ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kwa sababu asilimia 76.6 walipata

alama za wastani na zaidi. Chati Na. 2 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kiasilimia.





**Chati Na. 2:** *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, asilimia 47.6 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za juu kuanzia alama 3 hadi 4 kwa sababu walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ndogo ya *Aina za Maneno*.Watahiniwa hao waliweza kueleza maana ya vivumishi na viwakilishi na kutoa mifano miwili kwa kila moja. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza maana ya vivumishi kuwa ni *maneno yanayotoa maelezo zaidi kuhusu nomino au kiwakilishi* na kutoa mifano miwili kwa kutunga sentensi kisha kupigia mstari vivumishi hivyo. Mfano *Mtoto mzuri anacheza mpira, Yule mnene anakimbia.*

Katika sentensi "Mtoto mzuri anacheza mpira" mtahiniwa aliweza kuonesha neno *mzuri* kuwa ni kivumishi kwa sababu linaelezea zaidi juu ya nomino *mtoto* kama inavyoonekana kwenye sentensi. Vilevile, katika sentensi "Yule mnene anakimbia" mtahiniwa aliweza kuonesha neno *mnene* kuwa ni kivumishi kwani linaelezea zaidi kuhusu kiwakilishi *yule*. Aidha, alitoa maana ya viwakilishi kuwa ni *maneno yanayosimama badala ya nomino.* Mfano, *Wale wanaimba wimbo, Wao wanasoma kwa sauti*. Katika sentensi hizo viwakilishi *wale* na *wao* vinaweza kusimama badala ya nomino *wanakwaya* na *wanafunzi* mtawalia. Kwa ujumla, mtahiniwa huyo alijibu kulingana na matakwa ya swali kwa kutoa

maana na mifano miwili kwa kila dhana na hivyo kupata alama zote 4. Kielelezo Na. 2.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kueleza maana ya viwakilishi na vivumishi kwa usahihi kisha kutoa mifano miwili kwa kila moja.


2. a) Vivumishi. Ni Maneno yanayotoa sifa za kiwakilishi au nomino.
Mfano:-
(i) Mtoto mzuri anacheza mpira.
(ii) Yule Mnene anakimbia.

b) Viwakilishi. Ni Maneno yanayosimama badala ya nomino.
Mfano:-
(i) Wale wanaimba wimbo
(ii) Wao wanasoma kwa sauti.


**Kielelezo Na. 2.1:** Majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

Kielelezo Na. 2.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kutumia mifano miwili kwa kila moja, kueleza maana ya aina za maneno alizopewa ambazo ni: (a) Vivumishi na (b) Viwakilishi.

Vilevile, asilimia 29.0 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 2 hadi 2.5. Watahiniwa hao hawakuzingatia kikamilifu matakwa ya swali, kwa sababu baadhi yao walieleza maana bila kuweka mifano na wengine walieleza maana kwa usahihi ingawa mifano waliyotoa haikuwa sahihi. Aidha, wapo watahiniwa ambao walifanikiwa kueleza maana sahihi katika kipengele (a) pamoja na mifano na kushindwa kutoa maana na mifano katika kipengele (b).

Hata hivyo, asilimia 23.4 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 1.5. Baadhi ya watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada ya *Sarufi* hususan mada ndogo ya *Aina za Maneno* na wengine hawakuelewa matakwa ya swali. Baadhi yao walichanganya maana ya vivumishi, viwakilishi na vielezi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza kuwa vivumishi *ni maneno yanayosimama badala ya nomino* badala ya kueleza kuwa ni *maneno yanayotoa maelezo zaidi kuhusu nomino na viwakilishi* ilihali maneno yanayosimama badala ya nomino ni viwakilishi na si vivumishi. Vilevile, alitoa maana ya viwakilishi kuwa ni *maneno yanayoelezea zaidi jinsi*

*tendo lilivyotendeka* badala ya *maneno yanayosimama badala ya nomino*. Aidha, hakutoa mfano kama matakwa ya swali yalivyoelekeza hivyo kupata alama 0. Kielelezo Na. 2.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali vizuri na kupata alama hafifu.


2. (a) Vivumishi ni maneno yanayosimama badala ya nomino.
Mfano –
(b) Viwakilishi ni maneno yanayoelezea zaidi jinsi tendo lilivyotendeka.
Mfano –


**Kielelezo Na. 2.2** : Majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 2.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kueleza maana sahihi ya vivumishi na viwakilishi na kutoa mifano kulingana na matakwa ya swali.

### 2.1.3 Swali la 3: Uchambuzi wa Vifaa vya Mtaala wa Somo la Kiswahili

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uchambuzi wa Vifaa vya Mtaala wa Somo la Kiswahili*. Swali lililenga kupima maarifa ya mtahiniwa juu ya Uchambuzi wa Vifaa vya Mtaala wa somo la Kiswahili ambapo mtahiniwa alitakiwa kueleza kwa kifupi sifa nne za kitabu cha ziada.

Asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Kati yao asilimia 52.7 walipata alama za wastani na zaidi hivyo kufanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa kwa kiwango cha wastani.




**Chati Na. 3:** *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Watahiniwa 2,069 ambao ni sawa na asilimia 47.3 walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 1.5. Baadhi ya majibu ya watahiniwa hao yalidhihirisha kuwa, watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada ya *Uchambuzi wa Vifaa vya Mtaala wa Somo la Kiswahili* hivyo kushindwa kueleza kwa kifupi sifa mahsusi za kitabu cha ziada na kutoa maelezo kwa kubuni tu yaliyopelekea kupata alama hafifu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza sifa za kitabu cha ziada kuwa ni: *huwa na maarifa yanayohusu jamii inayotuzunguka, hakina mpangilio wa mada zinazofundishwa, hakipo kwenye mtaala na mara nyingi huwa ni kazi ya fasihi.* Vilevile, watahiniwa wengine walichanganya sifa za kitabu cha ziada na umuhimu wake kutokana na kutokuelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza kuwa *kitabu cha ziada kinamsaidia mwanafunzi kupata maarifa yanayoendana na maudhui aliyojifunza na humsaidia mwanafunzi kupata maelezo ya ziada kuhusiana na mada mbalimbali alizojifunza* na kupata alama 1.5. Kielelezo Na. 3.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali kwa usahihi kutokana na uelewa mdogo wa mada.

Q3. (i) Huwa na maarifa yanayoendana mazing-
ira au jamii inayotuzunguka; Kitabu
cha ziada huelezea zaidi namna watu
wanavyoishi katika jamii zao hivyo
watu husoma kwa lengo la kuongezea
maarifa tu.

(ii) Hakina mpangilio wa mada zitakazo
fundishwa; Kitabu cha ziada si kita
bu cha kufundishia hivyo chenyewe
hakijaorodhesha mada za somo kwa
ajiri ya kufundishia.


(iii) Hakipo kwenye mtaara; Kitabu cha
ziada hakipo katika mtaala unata
kiwa kufundishwa darasani ila
kinatumika kuongezea maarifa tu.

(iv) Mara nyingi huwa ni kazi ya fasihi;
Vitabu vingi vya ziada vinakuwa
kazi ya fasihi andishi. Mfano kita
bu cha NGOSWE PENZI KITOVU CHA
UZEMBE.

**Kielelezo Na. 3.1 :** Majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 3.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kueleza kwa kifupi sifa nne za kitabu cha ziada kutokana na kukosa maarifa ya kutosha juu ya mada ya *Uchambuzi wa Vifaa vya Mtaala wa Somo la Kiswahili*.

Kwa upande mwingine, asilimia 29.2 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za juu kuanzia 3 hadi 4 kwa sababu walielewa vizuri mada ya *Uchambuzi wa Vifaa vya Mtaala wa Somo la Kiswahili*. Watahiniwa hao waliweza kueleza kwa kifupi sifa tatu hadi nne za kitabu cha ziada kwa hoja kama : *kiwe na maudhui yanayoendana na muhtasari wa somo husika, kinatoa maelezo ya kina juu ya mada zote au baadhi ya mada zilizopo kwenye muhtasari wa somo, kiwe na lugha sanifu na fasaha inayoeleweka kwa wasomaji na kiwe na mazoezi ya wanafunzi ya kutosha.* Vilevile, watahiniwa wengine waliandika sifa nyingine kama vile *kitabu cha ziada kinatakiwa kuwa na utoshelevu wa michoro au picha zinazosadifu mada husika na kuzingatia utamaduni wa jamii husika/kisieleze mambo ambayo ni kinyume na utamaduni wa jamii husika*. Kielelezo Na. 3.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.



3 i) Kiwe na maudhui yanayoendana na
muhtasari wa Somo. Kitabu cha kiada kina
maudhui ambayo yanaendana na muhtasari
wa Somo husika japo kuwa yaweza kuwa
mengi au machache
ii) Kinatoa maelezo ya kina juu ya mada zilizo
po kwenye mhtasari wa Somo. Pia kitabu
au vitabu vya ziada hufafanua kwa kina
mada zinazopatikana kwenye mhtasari wa
Somo husika
iii) Kina lugha sanifu na fasaha inayoeleweka
kwa msomaji. Pia kitabu cha ziada hutumi
a lugha sanifu na fasaha inayoweza kuele
weka kwa msomaji.
iv) Kina mazoezi mengi ya kumpima mwanafunzi.
Pia kitabu cha ziada huwa na maswali
mengi kwa kila mada ambayo husaidia kupi
ma uelewa wa mwanafunzi na kupata tathmini
halisi ya Somo.

**Kielelezo Na. 3.2:** Majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi.


Kielelezo Na. 3.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeeleza sifa kuu nne za kitabu cha ziada kwa usahihi kutokana na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Uchambuzi wa Vifaa vya Mtaala wa Somo la Kiswahili*.

Aidha, asilimia 23.5 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 2 hadi 2.5 kwa sababu hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya *Uchambuzi wa Vifaa vya Mtaala wa Somo la Kiswahili*. Baadhi ya watahiniwa hao walieleza kwa kifupi sifa mbili badala ya nne na wengine walieleza sifa mbili za kitabu cha ziada na mbili za kitabu cha kiada hivyo kushindwa kupata alama za juu.

### 2.1.4 Swali la 4: Fasihi simulizi


Swali hili lilitoka katika mada ya *Fasihi Simulizi*. Swali lilimtaka mtahiniwa kutaja sifa kuu nne za fasihi simulizi. Asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Kati yao, asilimia 25.2 ya watahiniwa waliojibu

swali hili walipata alama za wastani na zaidi. Hivyo, kufanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vibaya kama inavyoonekana katika Chati Na. 4.




**Chati Na. 4:** *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Uchambuzi unaonesha kuwa, watahiniwa 3,269 sawa na asilimia 74.8 walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 1.5 kwa kuwa hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Fasihi simulizi* na kushindwa kutimiza matakwa ya swali. Wengi kati yao walishindwa kutofautisha kati ya sifa za fasihi simulizi, sifa za fasihi andishi na umuhimu wa fasihi simulizi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja umuhimu wa fasihi simulizi kuwa ni *huelimisha jamii, huburudisha jamii, hukuza lugha na Fasihi Simulizi ni chanzo cha ajira* badala ya kutaja sifa za fasihi simulizi ambazo ni: *kuwepo kwa utendaji, Kuwepo na mtendaji au fanani, Kuwepo kwa hadhira, Kuwepo kwa mandhari/mazingira pia kueleza kuwa fasihi hii ni kongwe, hubadilika kulingana na wakati pia huzaliwa hukua na hufa*. Mtahiniwa huyo alitaja umuhimu wa fasihi simulizi badala ya sifa za fasihi simulizi na hivyo kupata alama 0 kama inavyoonekana katika kielelezo Na. 4.1.



4. (i) Huelimisha jamii
(ii) Hukuza lugha
(iii) Huburudisha jamii
(iv) Chanzo cha ajira na kipato.

**Kielelezo Na. 4.1:** Majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 4.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutaja sifa kuu nne za fasihi simulizi badala yake akataja umuhimu wa fasihi simulizi katika jamii

Vilevile, watahiniwa 704 sawa na asilimia 16.1 walipata alama za wastani kuanzia 2 hadi 2.5 kwa kuwa hawakujibu swali hili kikamilifu. Baadhi yao walitaja sifa kuu mbili za Fasihi simulizi badala ya nne na wengine walitaja sifa sahihi mbili na kukosa zingine kutokana na kuchanganya sifa na umuhimu wa Fasihi Simulizi.

Hata hivyo, watahiniwa 398 sawa na asilimia 9.1 walipata alama za juu kuanzia 3 hadi 4. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Fashi simulizi* na walielewa mahitaji ya swali. Hivyo, waliweza kutaja kwa usahihi sifa kuu tatu hadi nne za Fasihi simulizi ambazo ni: *Kuwepo na utendaji, Kuwepo na mtendaji au fanani na hadhira, Kuwepo na mandhari/mazingira na hubadilika kulingana na wakati pia huzaliwa hukua na hufa*. Kielelezo Na. 4.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama za juu.


4. i) Utendaji
ii) Inafanani na hadhira.
iii) Inaendana na wakati na mazingira
iv) Inazaliwa, inakuwa, inaishi na inakufa.


**Kielelezo Na. 4.2:** Majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 4.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kutaja sifa kuu nne za fasihi simulizi kutokana na kuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Fasihi simulizi*.

### 2.1.5 Swali la 5: Zana za Kufundishia na Kujifunzia

Swali hili lilitungwa kutoka katika mada ya *Zana za Kufundishia na Kujifunzia*. Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa muhtasari mambo manne ya kuzingatia wakati wa kutengeneza zana za kufundishia na kujifunzia.


Swali lilijibiwa na asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani huu. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kwa kuwa asilimia 99.1 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 2 hadi 4. Chati Na. 5 inafafanua viwango vya kufaulu kwa asilimia.




**Chati Na. 5:** *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, asilimia 95.7 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za juu kuanzia 3 hadi 4 kwa sababu walikuwa na uelewa wa juu kuhusu mada ya *Zana za Kufundishia na Kujifunzia*. Hivyo, waliweza kueleza kwa muhtasari mambo matatu hadi manne ya kuzingatia wakati wa kutengeneza zana za kufundishia na kujifunzia. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza mambo ya kuzingatia kwa hoja kama: *kuzingatia/ kuangalia lengo mahsusi la somo, kuzingatia umri wa wanafunzi, kuzingatia uwezo wa wanafunzi* na *kuzingatia ukubwa wa darasa*. Aidha, watahiniwa wengine walitoa majibu kama vile; *maudhui ya mada ambayo mwalimu anatarajia kufundisha darasani, upatikanaji wa malighafi ya kutengenezea zana katika mazingira* na *hali ya wanafunzi mfano wenye mahitaji*

*maalum* n.k. Kielelezo Na. 5.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri na kupata alama za juu.


5 i) Kuangalia / kuzingatia lengo malususi. katika utengene
zaji wa zana lengo malususi lazima kulizingatia
ii) kuzingatia umri wa walengwa, pia utengenezaji
lazima kuhusisha walengwa umri wao mfano
darasa la kwanza hawezi kutumia zana hii
au darasa la saba hawezi kutumia zana hii
iii) kuzingatia uwezo wa kutumia darasani. pia
mwalimu lazima kutengeneza zana itayoweza
kutumika mfano kwa mwanafunzi
iv) kuzingatia ukubwa wa darasa. pia mwalimu
lazima kuangalia ukubwa wa darasa na zana
yenyewe


**Kielelezo Na. 5.1:** Majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 5.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeelezea kwa muhtasari mambo ya kuzingatia wakati wa kuandaa zana za kufundishia na kujifunzia kwa usahihi.

Vilevile, asilimia 3.4 ya watahiniwa walipata alama za wastani kuanzia 2 hadi 2.5 kwa sababu ya kuwa na maarifa ya wastani katika mada husika. Baadhi yao walieleza kwa muhtasari mambo mawili ya kuzingatia wakati wa kutengeneza zana za kufundishia na kujifunzia badala ya mambo manne na wengine walichanganya majibu sahihi na yasiyokuwa sahihi. Mfano, mtahiniwa mmoja alieleza mambo mawili ya kuzingatia wakati wa kutengeneza zana za kufundishia na kujifunzia pamoja na sifa mbili za zana hivyo kupata nusu ya swali.

Aidha, watahiniwa 39 sawa na asilimia 0.9 walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 1.5 kwa sababu baadhi yao hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Zana za Kufundishia na Kujifunzia* na wengine hawakuelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza juu ya hatua za kufuata wakati wa kutengeneza zana kwa hoja kama: *wazo, vifaa vya kutengeneza zana alivyo navyo, ujuzi na kuanza kutengeneza zana* badala ya mambo ya kuzingatia wakati wa kutengeneza zana za kufundishia na kujifunzia ambayo ni: *kuzingatia/ kuangalia lengo mahsusi la somo, kuzingatia umri wa wanafunzi, kuzingatia*

*uwezo wa wanafunzi na kuzingatia ukubwa wa darasa* na hivyo kupata alama 0. Kielelezo Na.5.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu kwa kushindwa kutoa hoja sahihi.


5. i) waro, Mwalimu lazima awe na waro ili awere kutengenera zana lazima awe nawaro.
ii) Makunzi / vifaa vya kutengenerezea, lazima Mwalimu awere kuwana vifaa vija kume za kutengenerea.
iii) Ujuzi, pia lazima awe na ujuzi wa kuwera kutengenera kile kitu anaeta fakiwa kutengenera.
iv) kuanza kutengenera akisha mali za kuwana vifaa hivyo ndipo amere kutengenera zana hiyo.


**Kielelezo Na. 5.2:** Majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 5.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeelezea kwa muhtasari hatua za kufuata wakati wa kutengeneza zana badala ya mambo ya kuzingatia wakati wa kutengeneza zana za kufundishia na kujifunzia.

### 2.1.6 Swali la 6: Utungaji


Swali lilitoka katika mada ya *Utungaji*. Swali lililenga kupima maarifa ya mtahiniwa juu ya utungaji ambapo mtahiniwa alitakiwa kuonesha sehemu kuu nne (4) za insha.

Watahiniwa wote waliofanya mtihani yaani asilimia 100 walijibu swali hili. Aidha, swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyofanywa vizuri kwani asilimia 99 ya watahiniwa walipata alama za wastani na zaidi. Chati Na. 6 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa katika asilimia.




**Chati Na. 6:** *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Asilimia 98.7 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za juu kuanzia 3 hadi 4 kwa sababu walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Utungaji* pamoja na kuelewa matakwa ya swali. Watahiniwa hao waliweza kutaja sehemu kuu tatu hadi nne za insha ambazo ni: *kichwa cha insha, utangulizi, kiini cha insha na hitimisho*. Kielelezo Na. 6.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za juu kwani aliweza kutaja sehemu za insha kwa usahihi.




06. Sehemu kuu za insha
(i) Kichwa cha insha
(ii) Utangulizi
(iii) Kiini cha insha.
(iv) Hitimisho

**Kielelezo Na. 6.1:** Majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 6.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuonesha sehemu kuu nne za insha kwa usahihi kutokana na kupata maarifa ya kutosha juu ya mada ya *Utungaji*.

Vilevile, watahiniwa 41 sawa na asilimia 0.9 walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 1.5 kutokana na kutokuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Utungaji*. Watahiniwa hao walishindwa kutaja sehemu kuu za insha badala yake, wapo

waliotaja mambo ya kuzingatia wakati wa kuandika insha na wengine walitaja mambo mengine yasiyohusiana kabisa na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kutaja sehemu kuu moja tu kwa usahihi ambayo ni *kichwa cha habari* na kupata alama 1. Aidha, sehemu nyingine tatu alizotaja hazikuwa sahihi ambazo ni *misamiati iliyopigiwa mistari, kuandika kwa kufuata aya* na *kusoma kwa makini insha hiyo* badala ya *utangulizi, kiini cha insha na hitimisho* kama inavyoonekana katika kielelezo Na. 6.2.


6 i) Kichwa cha habari
ii) Kuandika kwa kufuata aya.
iii) Misamiati iliyopigiwa mistari au kutole
2wa kwa wino
iv) Kusoma kwa Makini Insha hiyo.

**Kielelezo Na. 6.2:** Majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.


Kielelezo Na. 6.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuonesha sehemu moja ya insha badala ya nne kutokana na uelewa mdogo wa mada hivyo kupata alama hafifu.

Aidha, watahiniwa 14 ambao ni asilimia 0.3 walipata alama za wastani kuanzia 2 hadi 2.5. Wengi wao walitaja sehemu kuu mbili za insha badala ya nne na wengine walichanganya sehemu za insha na umuhimu wa insha.

### 2.1.7 Swali la 7: Maandalizi ya Kufundishia Somo la Kiswahili


Swali hili lilitoka katika mada za *Ufundishaji* hususan mada kuu ya *Maandalizi ya Kufundishia Somo la Kiswahili.* Swali lilikuwa na vipengele viwili ambapo lililenga kupima uelewa wa mtahiniwa juu ya mambo yanayopaswa kuoneshwa na mwalimu baada ya kufundisha katika (a) Tathmini na (b) Maoni.

Swali lilijibiwa na asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani. Kati yao, asilimia 81.7 walipata alama 2 hadi 4 na kufanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri. Chati Na. 7 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kiasilimia.




**Chati Na. 7**: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa 1,789 sawa na asilimia 40.9 walipata alama za juu kuanzia 3 hadi 4 kwa sababu ya uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Maandalizi ya Kufundishia Somo la Kiswahili* pamoja na kuzingatia matakwa ya swali. Watahiniwa hao, waliweza kufafanua kwa kifupi mambo mawili yanayopaswa kuoneshwa na mwalimu baada ya kufundisha katika vipengele vya *Tathmini* na *Maoni*. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua mambo yanayopaswa kuoneshwa na mwalimu katika kipengele cha *Tathmini* kuwa ni: *idadi ya wanafunzi walioelewa somo na ambao hawakuelewa somo* na *ikiwa lengo mahususi limefikiwa au halijafikiwa* na katika kipengele cha Maoni; *mwalimu aoneshe kipengele kinachofuata katika kipindi kingine na aoneshe mikakati itakayofanyika ili kusaidia wanafunzi ambao hawakuelewa.*Tofauti ya alama za watahiniwa katika kundi hili ilitokana na usahihi wa maelezo waliyoyatoa kwa kila kipengele. Kielelezo Na. 7.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kufafanua kwa kifupi na kwa usahihi mambo mawili yanayopaswa kuoneshwa na mwalimu katika kipengele cha *Tathmini* na *Maoni* baada ya kufundisha.



7. a) Tathmini
i) Idadi ya wanafunzi walioelewa somo na ambao hawajaelewa somo.
ii) Lengo mahususi limefikiwa au halijafikiwa.

b) Maoni
i) Kipengele kinachofuata katika kipindi kingine.
ii) Kama wapo wanafunzi ambao hawajaelewa somo mwalimu anapaswa kuonesha mikakati itakayofanyika ili kuwasaidia.

**Kielelezo Na. 7.1:** Majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi.


Kielelezo Na. 7.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kufafanua kwa kifupi mambo mawili yanayopaswa kuoneshwa na mwalimu baada ya kufundisha katika vipengele vya *Tathmini* na *Maoni*.

Hata hivyo, asilimia 40.8 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 2 hadi 2.5. Uchambuzi wa majibu ya baadhi ya watahiniwa unaonesha kuwa, hawakuelewa matakwa ya swali kikamilifu hivyo kueleza jambo moja ambalo mwalimu anapaswa kuonesha katika vipengele vya tathmini na maoni na wengine wakaonesha mambo mawili katika kipengele kimoja cha tathmini au maoni.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, asilimia 18.3 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 1.5. Katika kundi hili wapo ambao hawakuelewa matakwa ya swali hivyo kupata alama 0. Watahiniwa hao walishindwa kutofautisha kati ya mambo yanayopaswa kuoneshwa na mwalimu kwenye kipengele cha *Tathmini* na *Maoni* na njia za kufanya tathmini na maoni yanayotolewa katika Taasisi fulani kwa kuweka karatasi iliyoandikwa maoni mbalimbali yanayohusu taasisi hiyo kwenye sanduku maalum. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja njia za kufanya tathmini ambazo ni; *zoezi, majaribio, mitihani na mkoba wa kazi*.

Halikadhalika alieleza kuwa maoni ni *namna ya kuandika maoni na kuweka katika sanduku la maoni badala* ya kufafanua kwa kifupi mambo mawili yanayopaswa kuoneshwa na mwalimu baada ya kufundisha katika vipengele vya *Tathmini* na *Maoni* ambayo ni *idadi ya wanafunzi walioelewa somo na ambao hawakuelewa somo* na *ikiwa lengo mahususi limefikiwa au halijafikiwa* katika kipengele cha *Tathmini* na *mwalimu aoneshe kipengele kinachofuata katika*

*kipindi kingine na aoneshe mikakati itakayofanyika ili kusaidia wanafunzi ambao hawakuelewa* katika kipengele cha *Maoni*. Aidha, watahiniwa wengine walipata alama 1 kutokana na uelewa mdogo wa mada ya *Maandalizi ya Kufundishia Somo la Kiswahili*. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua jambo moja tu analoweza kufanya mwalimu katika kipengele cha tathmini na kushindwa mengine pamoja na kushindwa kutofautisha mambo yanayofanyika kwenye kipengele cha maoni na tathmini. Mambo aliyoyaeleza ni *kuuliza wanafunzi kama wameelewa* katika kipengele cha tathmini na *kupendekeza vitabu vitakavyotumika katika somo linalofuata pamoja na kuonesha kama lengo mahsusi limefanikiwa* katika kipengele cha maoni. Kielelezo Na. 7.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu kutokana na kujibu kinyume na matakwa ya swali.


7 (a) Tathmini
— Njia za kufanya Tathmini
• Kwa mfano
- Zoezi
— majaribio
— mitihani
— mkoba wa kazi

(b) Maoni
— Namna ya kuandika maoni ambayo huwekwa katika sanduku la maoni.


**Kielelezo Na. 7.2:** Majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 7.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kufafanua kwa kifupi mambo mawili yanayopaswa kuoneshwa na mwalimu katika kipengele cha *Tathmini* na *Maoni* baada ya kufundisha.

### 2.1.8 Swali la 8:Utungaji


Swali hili lilitoka katika mada ya *Utungaji*. Swali lilimtaka mtahiniwa kuorodhesha vipengele vinne muhimu katika uandishi wa kadi ya mwaliko.

Asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Miongoni mwao asilimia 92.4 walipata alama za wastani na zaidi na kufanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri. Chati Na. 8. inafafanua viwango vya kufaulu kwa asilimia.




**Chati Na. 8:** *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Watahiniwa 3237 sawa na asilimia 74.1 walipata alama za juu kuanzia 3 hadi 4 kwa sababu walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Utungaji* pamoja na kuelewa vyema matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kuorodhesha vipengele vyote vinne muhimu katika uandishi wa kadi ya mwaliko ambavyo ni: *kuonesha jina la mwandishi/mwalikaji, kuonesha jina la mwandikiwa/mwalikwa, kuonesha mahali na tarehe/siku* pamoja na *kuonesha mawasiliano kwa wasiofika.* Kielelezo Na. 8.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuorodhesha vipengele vinne muhimu katika uandishi wa kadi ya mwaliko.



8 i) Jina la mwandishi
ii) Jina la mwandikiwa.
iii) Mahali, muda na tarehe
iv) Mawasiliano kwa wasiofika.

**Kielelezo Na. 8.1:** Majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 8.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuorodhesha vipengele vinne muhimu katika uandishi wa kadi ya mwaliko na kupata alama za juu.

Vilevile, asilimia 18.3 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia alama 2 hadi 2.5 kwa sababu ya kuwa na uelewa wa wastani juu ya mada ya *Utungaji* hususan katika kipengele cha uandishi wa kadi ya mwaliko. Kwa mfano, baadhi yao waliweza kutaja vipengele 2 kwa usahihi na kukosa vipengele vingine na wengine walitaja vipengele 2 tu badala ya 4 na hivyo kushindwa kupata alama za juu.

Hata hivyo, watahiniwa 335 sawa na asilimia 7.7 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia alama 0 hadi 1.5 kwa kuwa hawakuwa na uelewa juu ya mada ya *Utungaji* hasa katika kipengele cha uandishi wa kadi za mwaliko. Watahiniwa hao walishindwa kutofautisha kati ya uandishi wa insha na kadi ya mwaliko. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa maelezo tu yanayohusiana na kadi ya mwaliko kama: *kadi ya mwaliko huwa na mwanzo wa kadi, maelezo ya kadi yenyewe, mwisho wa kadi na mawasiliano*. Aidha, watahiniwa wengine walieleza vipengele hivyo kuwa ni: *kichwa cha habari, utangulizi wa kadi, kiini au madhumuni ya kadi na hitimisho* badala ya kuorodhesha vipengele vinne muhimu katika uandishi wa kadi ya mwaliko ambavyo ni *kuonesha jina la mwandishi/mwalikaji, kuonesha jina la mwandikiwa/mwalikwa, kuonesha mahali na tarehe/siku* pamoja na *kuonesha mawasiliano kwa wasiofika.* Kielelezo Na. 8.2: ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuorodhesha vipengele vinne muhimu katika uandishi wa kadi ya mwaliko.



| | |
|---|---|
| 8 | Vipengele muhimu vya kadi ya mwaliko. |
| | - Mwanzo wa kadi |
| | - Kadi yenyewe. |
| | - Mwisho wa kadi |
| | - Mawasiliano. |


**Kielelezo Na. 8.2:** Majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 8.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuorodhesha vipengele vinne muhimu katika uandishi wa kadi ya mwaliko kutokana na uelewa mdogo wa mada.

### 2.1.9 Swali la 9: Maandalizi ya Ufundishaji

Swali lilihusu mada ya *Maandalizi ya kufundishia somo la Kiswahilii.* Swali hili lilikuwa na vipengele viwili; ambapo kipengele (a) kilimtaka mtahiniwa aeleze maana ya malengo mahsusi; na kipengele (b) ataje sifa tatu za malengo mahsusi.


Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wote waliofanya mtihani yaani asilimia 100 na ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kwa sababu asilimia 93.8 ya watahiniwa walipata alama 2 hadi 4. Chati Na. 9 inaonesha viwango vya kufaulu katika asilimia.




**Chati Na. 9:** *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Watahiniwa 3,736 sawa na asilimia 85.5 walijibu swali hili vizuri na kupata alama za juu kuanzia 3 hadi 4. Watahiniwa hao waliweza kukidhi matakwa ya swali kutokana na uelewa mkubwa waliokuwa nao juu ya mada ya *Maandalizi ya Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili*. Waliweza kueleza maana ya malengo mahsusi na kutaja sifa tatu za malengo mahsusi kwa ufasaha. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza maana ya malengo mahsusi kuwa ni; *tamko au kusudio linaloonesha badiliko la kitabia linalotarajiwa kuoneshwa na mwanafunzi mwishoni mwa somo*. Aidha, aliweza kutaja sifa tatu za malengo mahsusi ambazo ni; *Lengo mahsusi linapaswa litaje mlengwa (Mwanafunzi), liweze kupimika* na *liwe wazi*. Watahiniwa wengine waliweza kutaja sifa za malengo mahsusi kwa hoja kama: lifikiwe, litaje muda wa kufikiwa, liwe na

uhalisia n.k. Kielelezo 9.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi.


9. (a) Maana ya malengo mahususi
Ni malengo ambayo hutarajiwa na mwalimu kufikiwa na wanafunzi wake baada ya kujifunza mada ndogo fulani ndani ya kipindi darasani
Mfano; ndani ya kipindi cha dakika 40 kila mwanafunzi aweze kutaja vipengele vitano vinaunda barua ya kirafiki kwa usahihi.
(b) Sifa za malengo mahususi
(i) Lioneshe mlengwa/walengwa
(ii) Yaoneshe kiwango cha upimaji
(iii) Yaoneshe muda maalumu wa kufikiwa kwa malengo mahususi.


**Kielelezo Na. 9.1:** Majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 9.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeleza maana ya malengo mahsusi na kutaja sifa tatu za malengo mahsusi kwa usahihi.

Vilevile, asilimia 8.3 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama za wastani kuanzia 2 hadi 2.5 kwa kuwa hawakujibu swali kikamilifu. Baadhi yao, waliweza kueleza maana na kutaja sifa moja ya malengo mahsusi na kukosa sifa zingine na wengine walitaja sifa mbili tu bila kueleza maana.

Aidha, asilimia 6.2 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 1.5. Watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Maandalizi ya Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili*. Baadhi yao waliweza kuandika maana tu ya malengo mahsusi na kushindwa kuandika sifa zake na wengine waliweza kuandika kwa usahihi sifa moja na kupata alama 1 na wengine walijibu kinyume kabisa na matakwa ya swali na kupata alama 0. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa maana ya malengo mahsusi kuwa ni; *kipengele kinachopatikana katika mada kuu* na sifa zake ni *lazima yawe na mtiririko maalumu, lazima yatokane na mada kuu, lazima yafuate muda maalumu wakati wa kufundisha* badala ya kutoa maana ya malengo mahsusi kuwa ni: *tamko au kusudio linaloonesha badiliko la kitabia linalotarajiwa kuoneshwa na mwanafunzi mwishoni mwa somo* na kutaja sifa tatu kati ya zifuatazo: *Lengo mahsusi linapaswa litaje mlengwa (Mwanafunzi), liweze kupimika, liwe wazi na lifikiwe, litaje muda wa kufikia aidha liwe na uhalisia.*

Hata hivyo, watahiniwa wengine katika kundi hili walieleza kuwa *Malengo mahsusi huendana na malengo ya mtaala, humlenga mwanafunzi mmoja mmoja na hutofautiana katika kila mada* ambayo hayakuwa majibu sahihi. Kielelezo Na. 9.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu kutokana na uelewa mdogo juu ya mada ya Maandalizi ya Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili.


9. a) Malengo mahsusi ni vipengele vinachopatikana katika mada kuu.
b) i) lazima yaanze na mtiririko maalumu
ii) lazima yatokane na mada kuu.
iii) lazima yafuate muda maalumu-wakati wa kufundisha.


**Kielelezo Na. 9.2:** Majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 9.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuelezea maana ya malengo mahsusi na kutaja sifa tatu za malengo mahsusi kwa usahihi kutokana na uelewa mdogo wa mada ya *Maandalizi ya Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili*.

### 2.1.10 Swali la 10: Stadi za lugha

Swali hili lilitoka katika mada ya *Stadi za Lugha*. Swali lilikuwa na vipengele viwili ambapo mtahiniwa alitakiwa: (a) kueleza maana ya stadi za kuandika na (b) kuonesha aina mbili za mwandiko unaofudishwa katika shule za msingi.


Swali lilijibiwa na asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kwa sababu asilimia 70.2 ya watahiniwa walipata alama za wastani na zaidi. Chati Na. 10 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 10:** *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Asilimia 37.7 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 2 hadi 2.5 kutokana na kutokujibu kwa usahihi baadhi ya hoja. Watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Stadi za Lugha* kwa sababu waliweza kueleza maana ya stadi za kuandika bila kuonesha aina mbili za mwandiko unaofundishwa katika shule za msingi na wengine waliweza kuonesha aina mbili za mwandiko bila kueleza maana ya stadi za kuandika.

Vilevile, asilimia 32.5 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za juu kuanzia 3 hadi 4 kwa kuwa walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Stadi za Lugha*. Watahiniwa hao, walieleza maana ya stadi ya kuandika kuwa ni *uwezo au ujuzi wa kuumba na kuwasilisha alama au herufi katika uso wa kitu fulani kama vile ubao, karatasi na ardhini*. Pia, waliweza kuonesha aina mbili za mwandiko zinazofundishwa katika shule za msingi ambazo ni: *mwandiko wa chapa wenye vikonyo na mwandiko wa kuunga* huku wakishadidia majibu hayo kwa mifano. Tofauti ya alama za watahiniwa katika swali hili ilitokana na usahihi wa maelezo yaliyotolewa na watahiniwa kwa kila kipengele. Kielelezo Na. 10.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri.


10.

(a) Stadi za kuandika ni ule ujuzi au uwezo wa kuumba na kuwasilisha alama au herufi Katika wo wa kitu fulani, kwa mfano Katika Karatasi, Katika daftari, kibao, ardhini

(b) i/ Mwandiko chapa wenye vikonyo mfano. MAMA


ii/ Mwandiko wa kuunga Mfano Mama

**Kielelezo Na. 10.1:** Majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 10.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kutoa maana ya stadi za kuandika na kuonesha aina mbili za miandiko zinazofundishwa katika shule za msingi.

Hata hivyo, uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa asilimia 29.8 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 1.5. Watahiniwa hao, hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Stadi za Lugha*. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika maana ya stadi ya kuandika kuwa ni *aina ya stadi ya lugha ambayo huhusika na uandishi wa maneno kwa kutumia karatasi na kalamu* badala ya *uwezo wa kuchora michoro ya maandishi, alama au ishara zinazowakilisha sauti na ujumbe*. Vilevile, alitaja aina mbili za mwandiko unaofundishwa shule za msingi kuwa ni; *mwandiko wa kugandamizia na mwandiko wa kucharaza* badala ya *mwandiko wa chapa wenye vikonyo na mwandiko wa kuunga* hivyo kupata alama 1.

Hata hivyo watahiniwa wengine walijibu kinyume kabisa na matakwa ya swali na kupata alama 0. Mfano, mtahiniwa alieleza kuwa *stadi ya kuandika ni uwezo na ujuzi alionao mtu katika kushika kalamu* na kutaja aina mbili za mwandiko kuwa ni; *mwandiko wa wima na ulazo*. Kielelezo 10.2. ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi kutokana na uelewa mdogo wa mada.


10 Stadi ya kuandika.
Ni aina ya stadi ya lugha ambayo huhusika na uandishi wa maneno kwa kutumia karatasi na kalamu.

b) i) Mwandiko wa kugandamiza
ii) Mwandiko wa kuchaza

**Kielelezo Na. 10.2:** Majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 10.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kueleza maana ya stadi ya kuandika na kuonesha aina mbili za mwandiko unaofundishwa katika shule za msingi kwa usahihi.


### 2.2 SEHEMU B: Maswali ya Insha (Taaluma)

Sehemu hii ilikuwa na maswali matatu (3) ya insha ambayo yalitungwa kutoka katika mada za *Taaluma*. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali mawili (2). Kila swali lilikuwa na uzito wa alama kumi na tano (15) hivyo, kufanya sehemu hii kuwa na jumla ya alama thelathini (30). Aidha, kufaulu kwa watahiniwa kumegawanyika katika makundi matatu ambapo, mtahiniwa alipata kiwango hafifu cha kufaulu endapo alipata alama 0 hadi 5.5, 6 hadi 10 wastani na 10.5 hadi 15 kiwango kizuri.

### 2.2.1 Swali la 11: Fasihi simulizi

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Simulizi* na lililenga kupima maarifa ya mtahiniwa juu ya vitendawili. Swali lilimtaka mtahiniwa afafanue manufaa sita ya kufundisha na kujifunza vitendawili kwa wanafunzi wa shule za msingi.

Watahiniwa waliofanya swali hili ni 3811 sawa na asilimia 87.2. Kati yao, asilimia 99.4 walipata alama za wastani na zaidi na kufanya swali hili kuwa ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri. Chati Na. 11 inafafanua viwango vya kufaulu kwa asilimia.




**Chati Na. 11:** *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa 3,190 sawa na asilimia 83.7 walipata alama za juu kuanzia 10.5 hadi 15. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Fasihi Simulizi* hususan mada ndogo ya *Vitendawili*. Waliweza kufafanua manufaa manne hadi sita ya kufundisha na kujifunza vitendawili kwa wanafunzi wa shule za msingi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua hoja kama: *huburudisha wanafunzi, hurithisha kumbukumbu na kutunza amali za jamii, huelimisha jamii, hukuza lugha kwa wanafunzi na hukuza uwezo wa kufikiri kwa wanafunzi*. Pamoja na hayo, mtahiniwa huyo aliweza kutoa maelezo ya kina katika kufafanua hoja kwa kuzingatia kanuni za uandishi wa insha. Tofauti ya alama za watahiniwa katika kundi hili ilizingatia kiwango cha usahihi wa hoja na ufafanuzi uliotolewa na kila mtahiniwa. Kielelezo Na. 11.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama za juu.

11 Vitendawili ni usemi au semi zilizofumbwa ambazo hutolewa kwa hadhira ili ifumbue. Vitendawili pia hutumia lugha ya picha kama vile sitiari na huwa kuna pande mbili yaani mtegaji na mteguaji. Yafuatayo ni manufaa ya kufundisha na kujifunza vitendawili katika shule za msingi.

Huburudisha. Vitendawili huburudisha wanafunzi pale wanapojifunza na kufundishwa semi hizo, kwa mfano, popoo mbili za vuka mto – macho, mzungu kamlamba mjalua – chungu na moto, na hutembea akiliringa hata akiwa hatarini – kinyonga.


Hurithisha kumbukumbu na kutunza amali za jamii. Hivyo semi hizi huwawezesha wanafunzi kurithisha kumbukumbu na kutunza amali za jamii kama vile mila, desturi, lugha na utamaduni.

Huelimisha jamii. Wanafunzi wanapofundishwa au kujifunza husaidia kuelimisha jamii kwa mambo mbalimbali, mfano ukubwa wa pua – si wingi wa makamasi, mbili mbili hadi tanga – reli, pita huku nipite kule tumfinye mchawi – mkanda.

Hukuza lugha. Vitendawili pia husaidia kukuza lugha hiyo kuwa na msamiati wa kutosheleza kwa ajili ya matumizi ya kila siku, mfano, nakula lakini sishibi – hewa, mjomba hataki tuonane – kisogo, hesabu yako haina faida – nywele/mchanga.

Hukosoa na kuonya jamii. Faida nyingine ya vitendawili ni husaidia kuonya na kukosoa jamii pale inapoenda kinyume na taratibu za utamaduni wetu. Mfano, popoo mbili zavuka mto, maskini akipata – matako – hulia mbwata.

Hukuza uwezo wa kufikiri kwa mwanafunzi. Vitendawili humjengea uwezo mkubwa mwanafunzi wa



kufikiri na kukumbuka mambo kwa urahisi
katika ujifunzaji wake
Hivyo basi vitendawili vina manufaa makubwa
kwa wanafunzi kama yaliyobainishwa mfano,
kuelimisha jamii, Huburudisha jamii, kuhifadhi kumbu
kumbu, kurithisha amali za jamii, kukosoa na kuonya
jamii pamoja na kujenga mwanafunzi uwezo wa kufikiri
zaidi.


**Kielelezo Na. 11.1:** Majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 11.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kufafanua manufaa ya kufundisha na kujifunza vitendawili kwa wanafunzi wa shule za msingi.

Vilevile, asilimia 15.7 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama za wastani kuanzia 6 hadi 10. Watahiniwa hao hawakujibu kikamilifu kulingana na matakwa ya swali na wengine hawakufuata kanuni za kujibu maswali ya insha. Kwa mfano, baadhi yao walijibu swali kwa mtindo wa kuorodhesha hoja (manufaa ya vitendawili) na hivyo kukosa alama za utangulizi, kuelezea hoja na hitimisho na wengine walifafanua hoja mbili au tatu badala ya sita.

Hata hivyo, watahiniwa 21 sawa na asilimia 0.6 walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 5.5. Baadhi yao, hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Fasihi simulizi* hususan mada ndogo ya *Vitendawili* hivyo walishindwa kutoa hoja sahihi na kuzifafanua kikamilifu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua kuwa *vitendawili humsaidia mwanafunzi kushiriki katika kazi za uzalishaji, husaidia kuwepo na maelewano kwa wanafunzi waliogombana, huwafanya wanafunzi wafurahi na huwapa elimu* na kupata alama 4.5. Wengine walishindwa kuzingatia matakwa ya swali na hivyo kupata alama 0. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza sifa za vitendawili ambazo ni *vina pande mbili (yaani swali na jibu), huwa na fomula maalum yaani mwanzo kati na mwisho, vina matumizi ya picha, matumizi ya idadi ya vitu, hutumia lugha ya kishairi na huwa na maelezo mafupi mafupi* badala ya; *huburudisha wanafunzi, hurithisha kumbukumbu na kutunza amali za jamii, huelimisha jamii, hukuza lugha kwa*

*wanafunzi na hukuza uwezo wa kufikiri kwa wanafunzi*. Kielelezo Na. 11.2. ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kinyume na matakwa ya swali.



11. Vitendawili ni maneno ya fasihi ambayo watoto wanaulizwa halafu wanatoa majibu.

Yafuatayo ni manufaa ya Vitendawili

Vitendawili vina pande mbili yaani Swali na jibu lake. Lazima kuwe na watu wawili ambao mmoja anauliza na mwingine anajibu.

Huwa na fomula maalum, yaani huwa na mwanzo, kati na mwisho Mfano Swali -- Kitendawili, tega -- (kati), Kuku wangu katagia mibani nanasi.

Vinatumia Lugha ya picha, kwa mfano nyama nje ndani ngozi jibu lake, firigisi.

Vinaonesha idadi ya vitu kwa mfano popo mbili zavuka mto jibu lake ni macho. Kitendawili hicho kimetaja popo ambazo ni mbili

Hutumia Lugha ya kishairi, Lugha yake inakuwa na mapigo ya kimuziki hasa wakati wa kuuliza.

Vitendawili huwa na maelezo mafupi mafupi kama vile huku ng'o na huku ng'o jibu lake giza.

Hivyo basi ni muhimu kufundisha vitendawili kwa sababu vina manufaa hayo kwa wanafunzi wetu.

**Kielelezo Na. 11.2:** Majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.


Kielelezo Na. 11.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu kutokana na kufafanua sifa za vitendawili badala ya manufaa ya kufundisha na kujifunza vitendawili kwa wanafunzi wa shule za msingi.

.

### 2.2.2 Swali la 12: Utungaji

Swali lilitoka katika mada ya *Utungaji* na lililenga kupima maarifa ya mtahiniwa juu ya utungaji wa insha. Katika swali hili, mtahiniwa alitakiwa kuandika insha yenye maneno yasiyopungua 300 kuhusu "manufaa ya Tanzania kuwa nchi ya Viwanda".

Swali hili lilijibiwa na asilimia 82.2 ya watahiniwa waliofanya mtihani. Miongoni mwao, watahiniwa 3,553 sawa na asilimia 98.4 walipata alama za wastani na zaidi hivyo kufanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri. Utofauti wa alama kwa watahiniwa wa kundi hili ulizingatia kiwango cha usahihi wa hoja na ufafanuzi uliotolewa na kila mtahiniwa. Chati Na. 12 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa katika asilimia.




**Chati Na. 12:** *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Tathmini ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa inaonesha kuwa, asilimia 51.7 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 6 hadi 10. Watahiniwa hao walishindwa kuandika insha kikamilifu. Kwa mfano, wapo walioshindwa kufafanua hoja zao kwa kina, kuonesha kichwa cha insha na wengine kutokuandika sehemu ya utangulizi na hitimisho. Vilevile, wengine walishindwa kupanga vizuri hoja na kufuata kanuni za uandishi wa insha na hivyo kushindwa kupata alama za juu.

Vilevile, watahiniwa 1,678 sawa na asilimia 46.7 walijibu vizuri na kupata alama za juu kuanzia 10.5 hadi 15 kwa sababu walikuwa na maarifa ya kutosha

kuhusu mada ya *Utungaji* hususan mada ndogo ya *Uandishi wa Insha*. Vilevile, watahiniwa hao walifuata hatua zote za uandishi wa insha yaani utangulizi uliohusiana na swali, kiini na hitimisho. Aidha, walizingatia matumizi ya aya, alama muhimu za uandishi na hoja zilijengwa katika mtiririko unaoleta mantiki. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kuonesha kichwa cha insha ambacho ni *Tanzania ya Viwanda*, vilevile aliweza kueleza kwa kina manufaa ya Tanzania kuwa nchi ya viwanda kwa hoja kama: *kuliongezea taifa pato*, *wananchi kupata ajira, itasaidia nchi ya Tanzania kufikia uchumi wa kati, kutakuwa na uhakika wa soko kwa mazao mbalimbali* na *kutangaza jina la Tanzania katika soko la Dunia*.

Aidha, mtahiniwa huyo alionesha hitimisho linaloendana na insha husika pamoja na kutumia msamiati kwa usahihi. Tofauti ya alama za watahiniwa wa kundi hili ilizingatia kiwango cha usahihi wa hoja na ufafanuzi uliotolewa na kila mtahiniwa. Kielelezo Na. 12.1. ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama za juu.


12 TANZANIA YA VIWANDA

Viwanda ni sehemu maalum ambazo hutumika kuchakata malighafi kuwa bidhaa kwakutumia mashine mbalimbali za uchakataji. Mfano wa viwanda nchini Tanzania ni viwanda vya nguo, mafuta, urembo, magunia, sabuni pamoja na vitu vingine vingi. Yafuatayo ni manufaa ya Tanzania kuwa nchi ya viwanda.

Kuliongezea Taifa pato. Uwepo wa viwanda nchini husaidia kuliongezea Taifa pato kupitia ulipaji wa kodi mbalimbali serikalini kodi hizo hulipwa na wamiliki wa viwanda kama ilivyo ada kulipa kodi kwa serekali kwa mtu yeyote anayefanya biashara. Mfano, Kiwanda cha jambo kilichopo shinyanga hulipia kodi kwa taifa kila baada ya muda uliopangwa.

Ajira kwa wananchi. Uendeshaji wa viwanda huhitaji nguvukazi ili kuwepo kwa ufanisi wa utendaji kazi katika kiwanda hicho. Hivyo uwepo wa viwanda husaidia maelfu ya watanzania kupata ajira itakayowafaa katika maisha yao. Mfano Kiwanda cha Sod kilichopo Mwanza kimeajiri watumishi wa idara mbalimbali kwa idadi kubwa sana.

Husababisha nchi ya Tanzania kufikia uchumi wa kati. Hali hii hutokana na uzalishaji wa viwanda hivyo unaosababishwa na uzalishaji wa malighafi mbalimbali nchini Mfano Kilimo cha pamba, uzalishaji wa nguo na



12 uuzaji wa bidhaa hizo pamoja na kodi
kuchangia asilimia kubwa katika pato
la nchi na hivyo nchi kuwa na uchumi
wa kati.

Uhakika wa soko kwa mazao mbali-
mbali yanayolimwa nchini Tanzania. Kuto-
kana na uwepo wa viwanda, bidhaa mbali-
mbali zinazozalishwa au kulimwa zitapa-
ta soko la uhakika kwani viwanda uhit-
aji malighafi zitokanazo na kilimo na wa-
nanchi pia huhitaji bidhaa zitokanazo
na viwanda. Mfano watu hulima pamba
na mkonge na kuuzia viwanda na
viwanda huzalisha magunia na nguo
na kuwauzia wananchi.

Kutangaza jina la Tanzania katika
soko la dunia kutokana na bidhaa zinazo-
zalishwa na viwanda vya Tanzania na
hivyo nchi kuwa maarufu. Uwepo wa
viwanda hupeleka bidhaa zingine kwenda
nje ya nchi na hivyo kutangaza jina
la Tanzania. Mfano wa viwanda hivyo
ni vya nguo ambavyo huzalisha vitenge
ambavyo huuzwa nje ya nchi.

Kwahiyo uongozi wa nchi ya
Tanzania unatakiwa kufanya kila
mbinu zilizo halali katika kuha-
kikisha uchumi unapanda kwa njia
ya kuboresha viwanda na kuanzisha
na viwanda vingine vipya ili kuwa-
nufaisha wananchi wao.


**Kielelezo Na. 12.1:** Majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 12.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuandika vizuri insha inayohusu “manufaa ya Tanzania kuwa nchi ya viwanda”.

Hata hivyo, watahiniwa 3 ambao ni sawa na asilimia 1.6 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 5.5. Mtahiniwa aliyepata alama 0 hakuwa na uelewa juu ya mada ya *Utungaji* hususan uandishi wa insha. Mtahiniwa huyo alishindwa kuandika insha kwa kufuata kanuni za uandishi kama vile kutumia aya katika kuwasilisha hoja, alama mbalimbali za uandishi, kuandika kichwa cha insha, sehemu ya utangulizi na hitimisho. Hata

hivyo hakuweza kujenga hoja zake katika mtiririko unaoleta mantiki kwa msomaji. Kwa mfano, mtahiniwa aliandika insha kama kifungu cha habari chenye utangulizi, na kiini. Aidha, hakuweza kuandika manufaa ya Tanzania kuwa nchi ya viwanda; alitoa hoja kama; *kujenga standadi geji, Tanzania kuwa miongoni mwa nchi zenye viwanda, kuongezeka kwa megabaiti za umeme na kuongezeka kwa jiji la Dodoma* badala ya *kuliongezea taifa pato, wananchi kupata ajira, itasaidia nchi ya Tanzania kufikia uchumi wa kati, kutakuwa na uhakika wa soko kwa mazao mbalimbali na kutangaza jina la Tanzania katika soko la Dunia*. Pia, mtahiniwa huyo alishindwa kuonesha sehemu ya hitimisho.

Aidha, watahiniwa waliopata alama 1 hadi 5.5 walishindwa kufafanua hoja zao kikamilifu, wengi waliishia kutaja tu. Vilevile, walishindwa kuandika sehemu ya utangulizi na hitimisho inayoendana na insha husika pamoja na kutokutumia lugha fasaha. Kielelezo Na. 12.2. ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu kutokana na kutokuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada iliyotahiniwa.


12. Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo ziko
katika uchumi wa nchi ya viwanda, Tanzania
baada ya kujihusisha katika uchumi wa viwanda
imeweza kupata maendeleo mengi sana pamoja
na manufaa mbalimbali. Manufaa ambayo
Tanzania imeweza kupata ni pamoja ku-
jenga reli ya standard geji ambapo reli hiyo
imegharimu pesa kiasi kikubwa sana hivyo
basi ni moja ya manufaa ya Tanzania kuwa
nchi ya viwanda, kingine kutokana na kuonge-
zeka kwa mapato, mapato katika nchi ya
Tanzania yameongezeka juu sana baada
ya nchi kuingia au kuwa
miongoni mwa nchi za viwanda afri-
ka Mashariki pia Tanzania imenufai-
ika sana kuwa katika miongoni mwa
nchi za viwanda, imenufaika kuongezeka
kwa megabaiti za umeme nchini am-
bapo nchi baada ya kuwa katika nchi
za mfumo wa viwanda umeme umeon-
gezeka na kuwa katika kiwango cha
juu ambapo imeweza kutoa mahitaji ya
watanzania pia Tanzania imenufaika
kupata uchumi au kuwa nchi ya viwanda
kwa kuongezeka kwa jiji la dodoma na kuwa
miongoni mwa majiji nchini Tanzania pia
Tanzania kuwa nchi ya viwanda imeweza pia
kuinua uchumi wa nchi nzima ya Tanzania


**Kielelezo Na. 12.2:** Majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 12.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuandika insha kuhusu "manufaa ya Tanzania kuwa nchi ya viwanda" hivyo kupata alama hafifu.

### 2.2.3 Swali la 13: Sarufi

Swali lilitoka katika mada ya *Sarufi* na lilikuwa na vipengele vitatu ambapo mtahiniwa alipaswa kutumia mifano katika kubainisha tofauti na uhusiano uliopo kati ya jozi za aina za maneno zifuatazo: (a) Nomino na Vivumishi (b) Vitenzi na Vielezi (c) Vivumishi na Viwakilishi.

Idadi ya watahiniwa waliojibu swali hili ni 1332 sawa na asilimia 30.5 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Kati yao asilimia 82.8 walipata alama za wastani na zaidi hivyo kufanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri. Chati namba 13. inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 13:** *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, asilimia 64.3 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 6 hadi 10 kwa sababu walishindwa kutimiza matakwa ya swali kikamilifu. Baadhi yao waliweza kubainisha uhusiano uliopo baina ya jozi za maneno bila kuonesha mifano pamoja na kubainisha tofauti na wengine waliweza kubainisha tofauti kwa kutumia mifano bila kuonesha uhusiano uliopo baina ya jozi za aina za maneno zilizoulizwa.

Hata hivyo, watahiniwa 247 sawa na asilimia 18.5 walipata alama za juu kuanzia 10.5 hadi 15 kwa sababu walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada ya *Sarufi* hususan mada ndogo ya *Aina za Maneno* pamoja na kuelewa vyema matakwa ya swali. Watahiniwa hao, waliweza kutumia mifano katika kubainisha uhusiano na tofauti zilizopo baina ya jozi za maneno walizopewa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kubainisha uhusiano uliopo baina ya *Nomino* na *Vivumishi* kwa kueleza kuwa; *nomino huhusiana na kivumishi kwa sababu katika sentensi mpangilio wa maneno huanza na nomino kisha kufuatiwa na kivumishi ambacho hueleza zaidi kuhusu nomino*.

Aidha, aliweza kuonesha tofauti kati ya nomino na vivumishi kuwa *nomino ni aina za maneno yanayotaja kitu, mtu au hali Fulani, mfano Juma, bata, upepo na papasi ilihali vivumishi ni maneno yanayoelezea zaidi nomino mfano mzuri, mrefu na mdogo*. Vilevile, katika kipengele cha pili mtahiniwa huyo alieleza tofauti kati ya *Vitenzi* na *Vielezi* kuwa; *vitenzi ni maneno yanayotaja vitendo mfano piga, imba na omba* ila *vielezi ni maneno yanayoelezea zaidi namna tendo linavyofanyika kama vile polepole, upande upande* na *mjini*. Pia, aliweza kuonesha uhusiano kwa kueleza kuwa, *kama vielezi huelezea vitenzi ina maana lazima aina hizo za maneno ziwe sambamba katika sentensi*.

Hata hivyo, aliweza kubainisha uhusiano uliopo baina ya *Vivumishi* na *Viwakilishi* kuwa ni, *maneno yanayotumika kueleza zaidi juu ya nomino ni yaleyale yanayoweza kusimama badala ya nomino hizo ila itategemea limetumika wapi katika sentensi*. Tofauti ya alama za watahiniwa wa kundi hili ilizingatia kiwango cha usahihi wa hoja na ufafanuzi uliotolewa na kila mtahiniwa. Kielelezo Na. 13.1. ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

13. (a) • Utofauti uliopo kati ya Nomino na Vivumishi.

Nomino ni maneno au jina mfano Juma gari na kalamu lakini Vivumishi husifia nomino au jina mfano Juma mrefu – mrefu ni kivumishi, kalamu nzuri – nzuri ni kivumishi

• Uhusiano uliopo kati ya Nomino na Vivumishi

Nomino pamoja na Vivumishi vyote ni aina za maneno na hutegemeana kwani kivumishi hakiwezi kuwepo katika sentensi pasipo kuwepo na jina.

(b) • Utofauti uliopo kati ya vitenzi na vielezi

Vitenzi huelezea namna jambo lilivyo au ni aina ya neno inayoonesha kitendo, lakini Vielezi ni aina ya neno inayoelezea jinsi tendo lilivyofanyika

mfano: Vitenzi • Juma anakula

Neno "anakula" ni kitenzi

Mfano wa vielezi: • Juma anakula vizuri

Neno "vizuri" ni kielezi kinaelezea namna Juma alivyokula anakula.

(b) Uhusiano uliopo kati ya vitenzi na Vielezi

Vitenzi na vielezi hutegemeana kwani kisipokuwepo kitendo kielezi hakiwezi kuwepo kwani kazi yake huonekana kinapokuwepo kitenzi

Mfano: Juma anakula vizuri
T E

(c) Vivumishi na viwakilishi

• Utofauti wa vivumishi na viwakilishi ni:


Vivumishi husifu au kuvumisha nomino au kiwakilishi lakini Kiwakilishi huwakilisha nomino au jina hivyo tunaweza tumia kiwakilishi kuwakilisha jina au nomino.

Mfano wa viwakilishi.
• Mzuri amekuja

– Neno "Mzuri" ni kiwakilishi

Mfano wa vivumishi
• Mtoto mzuri amekuja

– Neno "Mzuri" ni kivumishi kimevumisha nomino ya mtoto



(c) • Uhusiano uliopo kati ya Vivumishi na Viwakilishi

Vivumishi pamoja na viwakilishi vinatage-
meana kwani vivumishi haviwezi kufanya
kazi yoyote pasipo kuwepo kiwakilishi au
nomino

Mfano: Huyu mrembo amekwenda wapi
W V


— Neno "Huyu" ni kiwakilishi na "mrembo" ni
kivumishi.

**Kielelezo Na. 13.1:** Majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 13.1 kinaonesha sapuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kutumia mfano kubainisha tofauti na uhusiano kati ya jozi za maneno zilizoainishwa katika swali hili kwa usahihi.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, asilimia 17.1 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 5.5. Watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Sarufi* na hawakuzingatia matakwa ya swali. Walishindwa kubainisha uhusiano na tofauti zilizopo baina ya jozi za aina za maneno walizopewa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza kuwa *nomino ni maneno au majina ya vitu fulani mfano Juma na Jeshi lakini vivumishi ni maneno yanayoonesha urejeshi wa mtenda mfano shambani* badala ya kueleza nomino kuwa ni *aina za maneno yanayotaja kitu, mtu au hali fulani mfano Juma, bata, upepo na papasi* ilihali *vivumishi ni maneno yanayoelezea zaidi nomino mfano mzuri, mrefu na mdogo*.

Vilevile, alieleza vitenzi kuwa ni *aina ya maneno inayoonesha jinsi tendo linavyotendeka, lilivyotendeka na linavyotendeka* na vielezi ni *aina ya maneno yanayoonesha jinsi tendo linavyotendeka* badala ya *vitenzi ni maneno yanayotaja vitendo mfano piga, imba na omba ila vielezi ni maneno yanayoelezea zaidi namna tendo linavyofanyika kama vile polepole, upande upande na mjini*. Pamoja na hayo, mtahiniwa huyo alishindwa kabisa kuonesha uhusiano uliopo, sehemu ya utangulizi na hitimisho la swali hivyo, kupata alama hafifu. Kielelezo Na. 13.1. ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu kutokana na kushindwa kutimiza matakwa ya swali.



13. (a) Nomino na Vivumishi.
Nomino ni maneno au majina ya vitu fulani mfano Juma, Jeshi
Lakini.
Vivumishi ni aina ya maneno ambayo huonesha urejeshi wa mtenda mfano shambani.

(b) Vitenzi na Vielezi.
Vitenzi ni aina ya maneno ambayo huonesha jinsi tendo lilivyotendeka, litakavyotendena na hata linavyotendeka mfano Anapenda, Alikwenda.
Lakini.
Vielezi ni aina ya maneno ambayo hueleza jinsi tukio lilivyotokea.
Mfano mzuri ni Kielezi cha sifa.
~~Lakini~~.

(c) Vivumishi na Viwakilishi.
Vivumishi ni aina ya maneno ambayo huonesha urejeshi wa mtenda mfano shambani.

**Kielelezo Na. 13.2:** Majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 13.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutumia mifano katika kubainisha tofauti na uhusiano uliopo baina ya *Nomino* na *Viwakilishi, Vitenzi* na *Vielezi* na *Vivumishi* na *Viwakilishi*.


## 2.3 SEHEMU C: Maswali ya Insha (Ufundishaji)

Sehemu hii ilikuwa na maswali matatu (3) ya insha ambayo yalitungwa kutoka katika mada za *Ufundishaji*. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali mawili (2). Kila swali lilikuwa na uzito wa alama kumi na tano (15) hivyo, kufanya sehemu hii kuwa na jumla ya alama thelathini (30). Aidha, kufaulu kwa watahiniwa kumegawanyika katika makundi matatu ambapo, mtahiniwa alipata kiwango hafifu cha kufaulu endapo alipata alama 0 hadi 5.5, 6 hadi 10 wastani na 10.5 hadi 15 kiwango kizuri.

### 2.3.1 Swali la 14: Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Kiswahili

Swali hili lilihusu mada ya *Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili* ambapo lilimtaka mtahiniwa kueleza faida sita za kutumia mbinu ya kazimradi katika kitendo cha ujifunzaji au ufundishaji.

Asilimia 77.4 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Aidha, swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kwa kuwa asilimia 87.0 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani na zaidi. Chati Na. 14 inaonesha viwango vya kufaulu kwa asilimia.




**Chati Na. 14:** *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Watahiniwa 1,482 sawa na asilimia 43.8 walifanya vizuri swali hili na kupata alama za juu kuanzia 10.5 hadi 15 kwa sababu walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili* pamoja na kuzingatia matakwa ya swali. Watahiniwa hao, waliweza kubainisha faida tano hadi sita za kutumia mbinu ya kazimradi katika kitendo cha ujifunzaji na ufundishaji kwa hoja kama: *mwanafunzi kujifunza kwa vitendo, huchochea udadisi, hujenga kumbukumbu ya kudumu, mwanafunzi hujifunza kutatua matatizo na hujipatia maarifa ya kutosha* n.k. Kielelezo Na.14.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kueleza faida za kutumia mbinu ya Kazimradi katika kitendo cha ujifunzaji na ufundishaji.

14 Kazimradi ni mojawapo ya mbinu ya kufundishia na kujifunzia ambayo mwalimu hutumia kwa kuwapa wanafunzi mada fulani na kuwataka waifanyie uchunguzi wa kina na kuwasilisha mrejesho. Zifuatazo ni faida za kutumia mbinu ya kazimradi katika kitendo cha ufundishaji na ujifunzaji.

Huwasaidia wanafunzi kujifunza kwa vitendo. Wanafunzi wanapofanya kazimradi huweza kujifunza mambo yaliyopo katika nadharia kwa vitendo, kwani huweza kupata muda wa kuhoji na kuchunguza mambo mbalimbali katika ujifunzaji wao.

Huchochea udadisi kwa wanafunzi katika kujifunza. Mbinu ya kazi mradi huwafanya wanafunzi kuwa wadadisi kwani huweza kuuliza maswali mbalimbali na wanakuwa na shauku ya kutaka kufahamu jambo kwa undani zaidi jambo ambalo huwafanya wawe wadadisi.

Huwajengea wanafunzi kumbukumbu ya kudumu. Mbinu ya kazimradi huwafanya wanafunzi wajifunze mambo mbalimbali kwa vitendo, hivyo huweza kukumbuka mambo mbalimbali, kwani huwashughulisha na kuwafanya wakumbuke.

Huwasaidia wanafunzi kuweza kutatua matatizo mbalimbali wanayokumbana nayo katika maisha yao ya kila siku; kazi mradi hutumia uchunguzi na utafiti wa kina ambao huwafanya wanafunzi wapate stadi mbalimbali wanazoweza kuzitumia katika kutatua matatizo katika maisha yao.

Wanafunzi huweza kujipatia maarifa ya kutosha. Kazimradi huweza kuwafanya wanafunzi kuwa na ujuzi na stadi kwani hujifunza mambo mbalimbali ya kiuchunguzi na kiutafiti ambayo hukuza kiwango chao cha uelewa.

Humrahisishia mwalimu mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Mwalimu anapotumia mbinu ya kazimradi huweza kumpunguzia maelezo mengi kwani wanafunzi huweza kupata muda wa kujifunza wenyewe na kumrahisishia mwalimu ufundishaji na ujifunzaji.

Hivyo basi, licha ya kazi mradi kuna mbinu nyingine zinazotumika katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kama vile nyimbo, maswali na majibu, onyesho mbinu igizo dhima na changanya kete.

**Kielelezo Na. 14.1:** Majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 14.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kubainisha faida tano za kutumia mbinu ya kazimradi katika kitendo cha ujifunzaji na ufundishaji kwa usahihi na kupata alama za juu.

Vilevile, asilimia 43.2 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 6 hadi 10. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa wastani hivyo, kushindwa kujibu swali kikamilifu. Kwa mfano, baadhi yao walieleza faida tatu au nne badala ya sita. Vilevile, watahiniwa wengine hawakuzingatia matakwa ya swali ambayo ni kujibu swali kwa mfumo wa insha.

Hata hivyo, asilimia 12.9 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 5.5. Watahiniwa waliopata alama 0 katika kundi hili, hawakuelewa matakwa ya swali kiasi cha kutoa majibu ambayo hayakuwa na uhusiano kabisa na swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja badala ya kuzungumzia kazimradi kama mbinu ya kufundishia na kujifunzia, alielezea kazimradi kama elimu ya kujitegemea shuleni na kueleza faida zake kuwa ni; *kupata kipato, chakula, kupendezesha mazingira ya shule, kuboresha miundombinu ya shule* na *kujenga nguvu kazi kwa vijana*.

Aidha, wapo watahiniwa waliopata alama kuanzia 1 hadi 5.5 kutokana na uelewa mdogo juu ya mada ya *Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili*. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alishindwa kueleza faida za kutumia mbinu ya kazimradi katika tendo la ufundishaji na ujifunzaji badala yake alieleza faida za jumla za matumizi ya mbinu mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji. Miongoni mwa majibu aliyoandika ni pamoja na: *inarahisisha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, humshirikisha mwanafunzi na huamsha ari ya wanafunzi kujifunza zaidi* n.k. Kielelezo Na.14.2. ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu kwa kukosa uelewa wa kutosha juu ya faida za kutumia mbinu ya kazimradi.

14 kazi mradi ni mbinu ambayo hutu
mika kwa ajili ya kufundishia na pia
katika kujifunzia mfano upandaji wa
mboga shuleni na pia upandaji wa
maua. Zifuatazo ni faida za kutumia
mbinu ya kazi mradi kwa kufundi
shia na kujifunzia mfano kupanda
nyasi miti,
kupendezesha shule. Ni faida ya ku
tumia mbinu ya kufundishia na kuji
funzia mbinu ya kazi mradi pale wa
nafunzi wanapojifunza kuhusu upanda
ji wa maua na kuweza kupendeze
sha shule.
Ni chanzo cha kipato ni faida
za kufundishia na kujifunzia kazi mra
di na kupeleka shule kuweza ku
pata kipato kutokana na kazi mradi
za wanafunzi na pia mwalimu.
kutupatia chakula ni faida moja
wapo ya kutumia mbinu ya kazi
mradi mfano katika shule mnejipu
nza namna ya kutengeneza mafu
ta kwa ajili ya upandaji wa mbo
ga za shule na kuweza kutupa
tia chakula na kupunguza ghara
ma pia
kuboresha muundo mbinu ni faida
za kufundishia pia na kujifunzia
kazi mradi mfano katika madara
sa kuna madawati mabovu na ku
weza kuweza mfano meza na kuwe
za kuboresha muundo mbinu ka
tika shule.
kumpatia maarifa mwanafunzi
ni faida ya kutumia mbinu ya
kazi mradi kwa mwanafunzi kwa
sababu inampatia maarifa zaidi kwa
akipika nyumbani na kuweza kupa
nya maarifa aliyojifunza akiwa shu
leni
kujenga nguvu kazi katika jamii
ni moja ya faida ya kutumia
mbinu ya kazi mradi kwa ajili ya
kufundishia na kujifunzia mwana
funzi anakuwa anapata nguvu ka
zi
Hivyo basi ni muhimu kufundi
sha na kutumia mbinu ya kazi
mradi kuweza kupunguza ghara
ma katika shule na pia kupu
nguza michezo kwa wanafunzi na
kujishughulisha katika shughuli mbalimbali.


**Kielelezo Na. 14.2:** Majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 14.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeelezea faida za elimu ya kujitegemea badala ya faida za kutumia mbinu ya kazimradi katika kitendo cha ujifunzaji na ufundishaji na kupata alama 0.

### 2.3.2 Swali la 15: Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Soma la Kiswahili

Swali lilitungwa kutoka katika mada ya *Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili*. Swali hili lilimtaka mtahiniwa kufafanua mbinu tano atakazotumia mwalimu katika kufundisha msamiati katika shule ya msingi.

Asilimia 78.2 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Aidha, asilimia 67.4 walipata alama za wastani na zaidi na kufanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa kwa kiwango cha wastani. Chati Na.15 inaonesha kiwango cha kufaulu katika asilimia.




**Chati Na. 15:** *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa 1,196 sawa na asilimia 35.0 walijibu swali hili vizuri na kupata alama za juu kuanzia 10.5 hadi 15 kwa sababu walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili* pamoja na kuelewa vizuri matakwa ya swali. Watahiniwa hao waliweza kufafanua mbinu nne hadi tano atakazotumia mwalimu katika kufundisha msamiati kwa shule ya msingi kwa hoja kama; *mbinu ya kutumia vitu halisi, kutumia vitendo, kutumia visawe vya maneno, kutumia vinyume vya maneno na kutumia maelezo* n.k. Kielelezo Na.15.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri na kupata alama za juu.

15. Msamiati, Ni jumla ya maneno yote yanayo unda lugha, mfano nomino, Vitenzi, vielezi, vivumishi na nyinginezo.
Msamiati huweza kuzuka kulingana na mataluwa ya watumiaji wa lugha na mahitaji yao kwa wakati, pia hutokana na matukio pamoja na Uchunguzi wa Kisayansi.
Zifuatazo ni mbinu atakazo zitumia mwalimu katika kufundisha msamiati katika shule za msingi:-
Vitu halisi, hivi ni vitu halisi kabisa kama vinavyo tumika na kuonekana. Lakini pia ni mbinu ya kufundisha msamiati k wa kuchukua vitu halisi na kuvileta darasani ili kufundishia msamiati husika. mfano kufundisha neno "Embe" ambapo utabeba tunda la embe na kufundishia darasani
vitendo, Hii pia ni mbinu ya kufundishia msamiati kwa wanafunzi, ambapo ~~mt~~ mwalimu atafanya kitendo chenye maana sawa na msamiati husika. mfano kufundishia neno Ruka. mwalimu ataruka na kuwaambia watoto hii ndio dhana ya Ruka.
Vinyume vya maneno mengine, Hii hutumiwa na mwalimu kufundishia msamiati baada ya kufundisha neno ambalo linakinyume chake. mfano kufundisha neno cheka utatumia kinyume chake ambacho ni Nuna.
Visawe, Hii ni njia ya kufundishia Msamiati kwa kutumia maneno yenye maana sawa na mengine ili wanafunzi wa

| | |
|---|---|
| 15 | wapate dhana iliyo kusudiwa mfano Kisawe |
| | Cha neno Tembo ni neno Ndovu, hivyo |
| | mwanafunzi kupata dhana ya msamiati huo |
| | Kutoa maana ya msamiati, Ni njia |
| | ya kufundisha msamiati ambapo mwali |
| | mu atawaeleza wanafunzi maana ya neno |
| | alilokusudia kulifundisha. mfano "Kulala" ni |
| | kitendo cha kupitiwa na usingizi n.k. |
| | Hivyo basi, msamiati ina faida nyi |
| | ngi sana kwa wanafunzi, kwani humsaidia |
| | kupanua lugha, humsaidia pia kupata |
| | dhana ya vitu mbali mbali. |

**Kielelezo Na. 15.1:** Majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 15.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kufafanua mbinu tano za kufundisha msamiati katika shule ya msingi kwa usahihi.

Vilevile, asilimia 32.4 walipata kiwango cha kufaulu cha wastani katika swali hili kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 10. Watahiniwa hao walipata alama za wastani kwa sababu hawakujibu swali kikamilifu. Wengi wao, walitaja mbinu za kufundisha msamiati bila kufafanua na wengine walifafanua hoja mbili au tatu badala ya tano.

Hata hivyo, watahiniwa 1,113 sawa na asilimia 32.6 walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 5.5 kwa sababu hawakuelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alishindwa kufafanua mbinu mahsusi atakazotumia mwalimu katika kufundisha msamiati badala yake alifafanua mbinu za jumla zinazoweza kutumika katika ufundishaji na ujifunzaji kwa hoja kama; *maswali na majibu, hojaji, mhadhara, onesho mbinu, majadiliano, kualika mgeni na matembezi ya galari* badala ya *mbinu ya kutumia vitu halisi, kutumia vitendo, kutumia visawe vya maneno, kutumia vinyume vya maneno, kutumia maelezo* na *kutumia maigizo*. Kielelezo Na. 15.2. ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa kuzingatia matakwa ya swali.

15\. Msamiati ni maneno ambayo yanalenga kitu fulani lakini yanakuwa yamefichwa ili kuweza kupata maana ya neno hilo. Mbinu zitakazo tumika na mwalimu katika kufundishwa msamiati katika shule ya msingi ni kama zifuatazo:-

Maswali na majibu; hii ni mbinu ambayo mwalimu anaweza kutumia katika kufundisha msamiati katika shule ya msingi, ambayo ~~am~~ mwalimu anauliza maswali wanafunzi wanajibu.

Hojajio; pia hii ni mbinu ambayo mwalimu anaweza kutumia katika kufundishwa msamiati shule ya msingi kwa kufanya mahojiano baina ya wanafunzi.

Mhadhara; vilevile mwalimu anaweza kutumia mbinu ya mhadhara kwa kufundishwa msamiati katika shule ya msingi. Mwalimu atafanya mhadhara mbele ya wanafunzi na kuanza kufundisha msamiati.

Mbinu shirikishi; hii ni mbinu ambayo mwalimu atatumia kufundisha msamiati kwa kushirikisha wanafunzi ambao anawafundisha hiyo mada.

Matembezi ya galani; vilevile hii ni mbinu moja wapo ya kufundisha msamiati ambayo itatumika kwa kufanya matembezi ya garali ili kufundisha msamiati.

Kwa hiyo; mwalimu anapaswa kutumia hizi mbinu kwa kufundisha msamiati katika shule ya msingi na kuleta uelewa kwa wanafunzi.


**Kielelezo Na. 15.2:** Majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.

**Kielelezo Na. 15.2** kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeelezea mbinu mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji badala ya mbinu atakazotumia mwalimu kufundisha msamiati katika shule ya msingi.

### 2.3.3 Swali la 16: Zana za Kufundishia na Kujifunzia

Swali lilihusu mada ya *Zana za Kufundishia na Kujifunzia* na lilimtaka mtahiniwa kubaini matumizi sita ya ubao wa kuandikia katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

Idadi ya watahiniwa waliojibu swali hili ni 1,935 sawa na asilimia 44.3 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Miongoni mwao, asilimia 94.2 walipata alama za wastani na zaidi. Hivyo, swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyofanywa vizuri. Chati Na. 16. inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa katika asilimia.





**Chati Na. 16:** *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Uchambuzi wa kina wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, asilimia 48.4 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani kati ya 6 hadi 10. Baadhi yao walishindwa kutimiza matakwa ya swali kwa sababu walijibu swali kwa kuorodhesha badala ya kueleza au kufafanua hoja na wengine walibainisha hoja pungufu ya sita zilizohitajika kwenye swali.

Hata hivyo, watahiniwa 887 ambao ni sawa na asilimia 45.8 walipata alama za juu kuanzia 10.5 hadi 15. Watahiniwa hao, walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Zana za Kufundishia somo la Kiswahili* hivyo waliweza kubainisha kwa usahihi matumizi manne hadi sita ya ubao wa kuandikia katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Halikadhalika, walielewa matakwa ya swali pamoja na kuzingatia kanuni za uandishi wa insha. Kwa mfano, mtahiniwa


mmoja alibainisha matumizi sita ya ubao kwa hoja kama: *hutumika kama zana ya kufundishia na kujifunzia stadi ya kuandika, hutumika kuandika nukuu za somo, hutumika kuandika tarehe ya siku husika*, *kuandika mazoezi mbalimbali ya wanafunzi, hutumika kuchora michoro mbalimbali na hutumika kuandika jina la somo* na *mada inayofundishwa*. Kielelezo Na.16.1ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri na kupata alama za juu.


16: Ubao wa kuandikia ni kitu bapa chenye nyuso au sehemu ya ukuta yenye nyuso iliyopakwa kwa rangi nyeusi kwa ajili ya kuandika, kuchora maumbo mbalimbali kama vile alama, herufi, namba. Ubao huu unaweza kuwa kwenye ukuta wa jengo au wa samani lakini lazima ukidhi viwango vya kutumika.

Ubao wa kuandikia una matumizi mbalimbali katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji matumizi hayo ni kama yafuatayo;-

Hutumika kama zana ya kufundishia na kujifunzia stadi ya kuandika katika stadi hii mwanafunzi atajifunza kupitia mbalimbali ambazo ni kuandika hewani, kwenye mchanga, daftarini na ubaoni hivyo ubao huo hutumika katika kufundisha stadi hii.

Humsaidia mwalimu kuandika nukuu za somo ili wanafunzi waweze kuandika hivyo ubao huo hutumika kwa ajili ya kazi hiyo mwalimu ataandika nukuu zake huku wanafunzi wakiandika pia daftarini.



16. Humsaidia mwalimu kuandika tarehe ya siku ambayo anafundisha ni wajibu wa mwalimu kuandika tarehe aliyofundisha vile vile na Wanafunzi ambao walikuwa hawajui tarehe Waweze kuifahamu.

Humsaidia mwalimu kuandika zoezi, jaribio au mtihani wakati anataka kupima wanafunzi wake kuhusu mada alizofundisha ili kila mwanafunzi aweze kusoma na kuandika mwenyewe maneno yaliyoandikwa.

Hutumika kuandika mada na somo linalofundishwa ndani ya kipindi husika hizi taarifa muhimu mwanafunzi kuzifahamu kwani ni rahisi kutambua mwanzo mpya wa mada nyingine vilevile ni somo gani linapaswa kufundishwa kwa muda huo.

Hutumika kubandika chati za michoro mbalimbali wakati wa ufundishaji vilevile utachora michoro kwenye ubao kutokana na mada unayofundisha hata wakati unapofanya masahihisho ya kazi mbali mbali huandikwa ubaoni.


Kwa ujumla ubao wa kuandikia ni zana msingi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kama jinsi matumizi yake yameelezwa juu lakini pamoja na hayo kuna changamoto za kutumia ubao kama vile maandishi kutoonekana kutokana na uchakavu wa ubao, Wanafunzi Jumuishi ndani ya darasa moja ambao wengine hawawezi kuona.

**Kielelezo Na. 16.1:** Majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 16.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeweza kubainisha matumizi sita ya ubao wa kuandikia katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kwa usahihi.

Ingawa kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri, baadhi ya watahiniwa walipata alama hafifu kuanzia 1 hadi 5.5 ambao ni sawa na asilimia 5.7 ya watahiniwa wote waliojibu swali hili. Watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Zana za Kufundishia na Kujifunzia* pamoja na kutokuzingatia matakwa ya swali. Baadhi yao walishindwa kutofautisha kati ya matumizi ya ubao na faida za ubao wa kuandikia katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza kuwa *husaidia kuwajengea wanafunzi kumbukumbu, husaidia mwalimu kupangilia vizuri kazi na husaidia mwanafunzi kuona maandishi.* Kielelezo Na. 16.2 ni sampuli ya

majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kufafanua matumizi ya ubao katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.



16. Ubao wa kufundishia na kujifunzia, ni kifaa ambacho huwasilisha tendo zima la ufundishaji na ujifunzaji kwa mwalimu na mwanafunzi. Pia kuna matumizi mbalimbali ya ubao katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji.

Yafuatayo ni baadhi ya matumizi ya ubao katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji kama ifuatavyo

Husaidia kurahisisha tendo la kufundisha na ujifunzaji; hii ni kwamba endapo ubao utakuwa ni wa kuonekana vizuri kwa mwalimu na mwanafunzi itasaidia kurahisisha kujifunza kwa ufanisi.

Husaidia wanafunzi kuona maandishi kwa usahihi na kuyaandika vizuri; pia kutokana na uwepo wa ubao wa kufundishia na kujifunzia hivyo kupelekea wanafunzi kuweza kuona maandishi kwa usahihi.

Husaidia mwalimu kupangilia vizuri kazi yake ubaoni; pia katika mchakato mzima wa kuandika ubaoni humsaidia mwalimu kuweza kupangilia kazi yake ubaoni vizuri kutokana na kugawa ubao vizuri.

Husaidia mwalimu kwa kufuata mtiririko mzuri; hii ni kutokana na kuweza kuandika mtiririko wake kwa mtiririko mzuri katika mchakato mzima wa ufundishaji wa ujifunzaji kwa wanafunzi katika darasa husika.

Husaidia wanafunzi kuweza kujifunza kwa ufanisi zaidi; hii ni kutokana na kuwa kile kinachoandikwa ubaoni na mwalimu wakati wa kufundisha mwanafunzi anakiona na kukiona vizuri hivyo kusaidia kuweza kujifunza kwa ufanisi.

Husaidia wanafunzi kuwajengea hali ya kumbukumbu ya walichojifunza; ubao kama ilivyo zana inayorahisisha tendo la ufundishaji na ujifunzaji kwa mwalimu na mwanafunzi hivyo kuwasaidia wanafunzi katika kujenga kumbukumbu kwa sababu ya kuona na kutumia milango ya fahamu katika kujifunza.

Hivyo basi, ni dhahiri kuwa ubao una matumizi mbalimbali katika ufundishaji na ujifunzaji. Mfano wa matumizi hayo ni kama kusaidia kurahisisha tendo la ufundishaji na kusaidia kuweza kuwajengea kumbukumbu wanafunzi ya walichojifunza.

**Kielelezo Na. 16.2:** Majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.

Kielelezo Na. 16.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefafanua umuhimu wa ubao badala ya matumizi ya ubao katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

## 3.0 UCHAMBUZI WA KUFAULU KWA WATAHINIWA KWA MADA

Mtihani wa 621 Kiswahili ulikuwa na maswali (16) yaliyotoka katika mada ya *Zana za Kufundishia na Kujifunzia, Utungaji, Sarufi, Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Kiswahili, Stadi za Lugha, Maandalizi ya Kufundishia Somo la Kiswahili, Fasihi Simulizi* na *Uchambuzi wa Vifaa vya Mtaala wa Kiswahili.*

Uchambuzi wa kufaulu kwa watahiniwa katika mada hizo unaonesha kuwa, watahiniwa wamefanya vizuri katika mada 5 ambazo ni sawa na asilimia 62.5 ya mada zilizotahiniwa. Mada hizo ni *Zana za Kufundishia na Kujifunzia (96.7%), Utungaji (96.6%), Sarufi (79.5%), Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Kiswahili (77.5%)* na *Stadi za Lugha (70.2%).* Watahiniwa walipata kiwango kizuri cha kufaulu katika mada zilizotajwa kwa sababu walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada hizo na utambuzi sahihi wa matakwa ya kila swali lililoulizwa kutoka katika mada hizo. Hali kadhalika, wengi wao waliweza kujieleza vizuri kwa lugha inayoeleweka, kujenga hoja vizuri katika mtiririko unaoleta mantiki pamoja na kufuata taratibu na kanuni za uandishi hususan katika maswali ya insha.

Aidha, watahiniwa walipata kiwango cha kufaulu cha wastani katika mada 4 amabazo ni sawa na asilimia 37.5. mada hizo ni *Maandalizi ya Kufundishia Somo la Kiswahili (66.9%), Fasihi Simulizi (62.3%)* na *Uchambuzi wa Vifaa vya Mtaala wa Kiswahili (52.5%)* Watahiniwa walifaulu kwa kiwango cha wastani katika mada zilizotajwa kutokana na uelewa wa wastani wa mada zilizotahiniwa na kutofuata kanuni za uandishi hususan katika maswali ya insha. Mchanganuo wa viwango vya kufaulu kwa watahiniwa kwa kila mada umefafanuliwa katika viambatisho A na B.

Kwa ujumla, kiwango cha kufaulu cha watahiniwa kwa somo hili ni kizuri kwa sababu asilimia 99.98 ya watahiniwa waliofanya mtihani walifaulu. Hali hii inaonesha kuwa, zaidi ya theluthi mbili (2/3) ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walikuwa na uelewa mzuri wa mada mbalimbali zilizotahiniwa.

## 4.0 HITIMISHO

Kwa ujumla, mtihani wa 621 Kiswahili kwa mwaka 2019 ulizingatia muhtasari wa somo la Kiswahili. Takribani majazi yote ya nyanja za utambuzi kama vile maarifa, ufahamu, matumizi, uchambuzi, uundaji na tathmini zilijidhihirisha katika mtihani huo. Aidha, kiwango cha kufaulu kwa ujumla kilikuwa kizuri kwa kuwa zaidi ya theluthi mbili 2/3 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walifaulu kwa asilimia 99.98.

Hata hivyo, uchambuzi uliofanyika ulibaini kuwapo kwa changamoto mbalimbali kwa baadhi ya watahiniwa zilizosababisha kushindwa kufanya vizuri. Miongoni mwa changamoto hizo ni; uelewa mdogo wa matakwa ya swali, uelewa mdogo wa mada zilizotahiniwa, kujibu maswali kwa kutokuzingatia matakwa ya swali na uelewa mdogo wa matumizi ya alama za uakifishaji sambamba na kushindwa kuandika insha zenye mtiririko unaoleta mantiki. Changamoto nyingine iliyobainika ni baadhi ya watahiniwa kushindwa kutoa mifano sahihi ya kushadidia majibu waliyotoa.

Hivyo, Baraza la Mitihani la Tanzania linatarajia kuwa, changamoto hizo zitatia chachu kwa wakufunzi na walimu tarajali wa somo hili katika kuelewa kasoro zinazofanywa na baadhi ya watahiniwa ambazo husababisha washindwe kujibu vizuri maswali. Kisha, wakufunzi na walimu tarajali waone kuwa kuna haja ya kurekebisha kasoro hizo zilizobainika kwa baadhi ya watahiniwa wa somo hili. Aidha, taarifa hii itazidi kuchochea ari ya wakufunzi katika kufundisha, kutunga na kusahihisha mazoezi na mitihani mbalimbali ili kuzidi kuinua kiwango cha kufaulu. Vilevile, walimu tarajali wanatarajiwa kuonesha hamasa na ari ya kutaka kuijua na kuimudu lugha ya Kiswahili ambayo inazidi kuenea kwa kasi kote ulimwenguni ili wajijengee umahiri katika kujieleza kwa kujiamni huku wakijivunia kutumia lugha hii.

## 5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

Ili kuzidi kuinua kiwango cha kufaulu katika somo hili, inapendekezwa mambo yafuatayo yazingatiwe:

(a) Mbinu zaidi ya moja zitumike katika ufundishaji na ujifunzaji vyuoni, ili kusaidia wanachuo kuelewa dhana mbalimbali kwa urahisi ikilinganishwa na matumizi ya mbinu ya aina moja.

(b) Wakufunzi watilie maanani katika kuwafundisha na kuwasisitiza walimu tarajali juu ya matumizi sahihi ya alama za uakifishaji sambamba na uandishi wa insha zenye mtitririko wenye kuleta mantiki. Hii itazidi kuchochea kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa ambao wamepata alama pungufu kwa kuandika insha zisizo na mtiririko mzuri.

(c) Kuhakikisha kuwa, mada zote zilizoainishwa katika muhtasari wa 621 Kiswahili zinafundishwa kikamilifu. Mbinu za kujifunzia zizingatie ushiriki wa wanafunzi zaidi.

(d) Wakufunzi wapewe mafunzo kazini ya mara kwa mara ambayo yatasaidia katika kubuni mbinu mpya za kufundisha mada zinazoonekana kuwa ngumu kwa wanafunzi.

(e) Taasisi ya Elimu Tanzania ihakikishe kuwepo kwa kitabu kimoja au viwili vya kiada vya somo la 621 Kiswahili vyenye maudhui ya mada zote zinazofundishwa ngazi ya Ualimu cheti ili kusaidia wanafunzi.

(f) Wakufunzi wawasaidie walimu tarajali katika kubuni mbinu bora za kujisomea kwa kina kabla ya kufanya mtihani.

(g) Wakufunzi wanasisitizwa kutumia mbinu za maswali na majibu, majadiliano ya vikundi na bungua bongo katika kufundisha mada ya *Uchambuzi wa Vifaa vya Mtaala wa Kiswahili* ili kuwafanya walimu tarajali kuwa mahiri zaidi katika mada hiyo.

**KIAMBATISHO A**

## MUHTASARI WA UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU CHA WATAHINIWA KATIKA KILA MADA

| Na | Mada | 2019 | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Namba ya swali | Viwango vya Kufaulu (%) | | Maoni |
| | | | 40 na Zaidi | Wastani | |
| 1. | Zana za Kufundishia na Kujifunzia | 5 | 99.1 | 96.7 | Vizuri |
| | | 16 | 94.2 | | |
| 2. | Utungaji | 6 | 99.1 | 96.6 | Vizuri |
| | | 8 | 92.4 | | |
| | | 12 | 98.4 | | |
| 3. | Sarufi | 2 | 76.6 | 79.7 | Vizuri |
| | | 13 | 82.8 | | |
| 4. | Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili | 14 | 87.6 | 77.5 | Vizuri |
| | | 15 | 67.4 | | |
| 5. | Stadi za Lugha | 10 | 70.2 | 70.2 | Vizuri |
| 6. | Maandalizi ya Kufundishia Somo la Kiswahili | 1 | 25.1 | 66.9 | Wastani |
| | | 7 | 81.7 | | |
| | | 9 | 93.8 | | |
| 7. | Fasihi Simulizi | 4 | 25.1 | 62.3 | Wastani |
| | | 11 | 81.7 | | |
| 8. | Uchambuzi wa Vifaa vya Mtaala wa Kiswahili | 3 | 52.5 | 52.5 | Wastani |

**KIAMBATISHO B**

**KIWANGO CHA KUFAULU CHA MADA KWA MWAKA 2019**

